**WIZARA YA MAJI NA USAFI**

**MRADI WA USALAMA WA MAJI NA USTAHIMILIVU WA HALI YA HEWA NCHINI KENYA (KWSRP) -HAWAMU YA KWANZA**

**UKAGUZI NA USASISHAJI WA MPANGO WA UHAMISHAJI (MUU) KWA AJILI YA MRADI WA UMWAGILIAJI WA LOWER NZOIA (MULN) NA MIJENGO YA KINGA DHIDI YA MAFURIKO NZOIA**

**RIPOTI YA MWISHO YA MPANGO WA UHAMISHAJI**

**(MUU III) – SEHEMU YA KWANZA YA KUZUIA MAJI**

**APRILI 2020**

**RIPOTI YA MWISHO**

**IMETAYARISHWA NA**


Southern Delta INTERNATIONAL

**Nextgen Mall, off Mombasa Road**

**Mombasa Road, South C**

**Nairobi, Kenya**

**Tel: +254 20 4158956 | +254 721 406361**

**Email: info@thesdi.net**

**Website:** www.thesdi.net

**NA**

**Stroutel Engineering**

Innovative Engineering

# YALIYOMO


| | | | |
|---|---|---|---|
| **1** | | **MUHKTASARI** | **1-1** |
| **1** | | **UFUPISHO** | **1-6** |
| | 1.1 | Utambulisho | 1-6 |
| | 1.1.1 | Mamlaka ya Ripoti | 1-6 |
| | 1.1.2 | Asili ya Mradi | 1-6 |
| | 1.2 | Maelezo ya Mradi | 1-7 |
| | 1.2.1 | Eneo la Umwagiliaji | 1-7 |
| | 1.2.2 | Sehemu ya Awamu ya kwanza ya Mradi wa Umwagiliaji wa Lower Nzoia | 1-7 |
| | 1.2.3 | Sehemu ya Majengo ya Kinga Dhidi ya Mafuriko ya Nzoia | 1-8 |
| | 1.3 | Wanufaika wa Mradi wa Lower Nzoia | 1-8 |
| | 1.4 | Malengo ya Mpango wa Utekelezi wa Uhamishwaji | 1-8 |
| | 1.5 | Wigo wa Mpango wa Utekelezaji uhamishwaji (MUU) | 1-9 |
| | 1.6 | Miundombinu ya mradi ambayo itaathiri mali | 1-10 |
| | 1.7 | Utafiti wa Kijamii na Kiuchumi na Matokeo | 1-10 |
| | 1.7.1 | Utafiti wa Kijamii na Kiuchumi | 1-10 |
| | 1.7.2 | Matokeo ya Utafiti wa Kijamii na Kiuchumi | 1-11 |
| | 1.8 | Utafiti wa sensa na Matokeo | 1-13 |
| | 1.8.1 | Utafiti wa sensa/Utafiti | 1-13 |
| | 1.8.2 | Matokeo ya Sensa | 1-14 |
| | 1.9 | Mikutano ya Mashauriano ya wadau na watu waliyoathirika na mradi | 1-16 |
| | 1.9.1 | Wito wa hisani | 1-17 |
| | 1.9.2 | Mkutano wa wadau na viongozi na utawala wa mitaa | 1-17 |
| | 1.9.3 | Mikutano ya kijamii ya utambulisho na uhamasishaji | 1-17 |
| | 1.9.4 | Mkutano wa maendeleo na machifu wa kata | 1-19 |
| | 1.9.5 | Mkutano wa mashauriano kwa ajili ya kuanzish | 1-19 |
| | 1.10 | Tarehe ya Mwisho | 1-20 |
| | 1.11 | Sera ya uhamishaji na haki stahiki | 1-20 |
| | 1.12 | Wasiwasi wa watu waliotharika na mradi, WWM | 1-20 |
| | 1.13 | Muhutasari wa athari za mradi na hatua za kukabiliana nazo | 1-21 |
| | 1.14 | Vigezo vya kustahiki fidia | 1-25 |
| | 1.15 | Thamani, Fidia na Haki | 1-25 |
| | 1.15.1 | Kuweka thamani ya mali | 1-25 |
| | 1.15.2 | Ustahiki | 1-25 |
| | 1.16 | Kupunguza gharama ya uhamishaji | 31 |
| | 1.17 | Mfumo wa kitaasisi wa utekelezaji wa MUU | 31 |
| | 1.17.1 | Kamati za uhamishaji na Fidia za Kaunti ndogo (KUFKNs) | 31 |
| | 1.17.2 | Kamati za kata za uhamishaji na fidia (LRCCs) | 32 |

1.18 Kushughulikia malalamiko 33
1.18.1 Ngazi ya kwanza: Kamati ya mtaa 34
1.18.2 Ngazi ya pili: Kamati ya Kaunti 35
1.18.3 Ngazi ya tatu: Kamati ya mradi 36

1.19 Uhamishwaji wa kaya zilizotengwa kabisa KZ 37

1.20 MMU III Makadirio ya jumla ya gharama 38

1.21 Urejeshaji wa hali ya Maisha 39
1.21.1 Kanuni muhimu zinazoongoza mpango wa marejesho ya hali za maisha 39
1.21.2 Mpango uliopendekezwa wa urejeshaji hali za maisha 39
1.21.3 Mpango wa urejeshaji hali za maisha (MUHM) makadirio ya gharama 40

1.22 Muhtasari wa matokeo ya utafiti wa MUU 40

1.23 Utafiti wa thamani 42

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BKU | Bodi ya Kitaifa Umwagiliaji |
| CWMU | Chama cha Watumizi wa Maji ya Umwagiliaji |
| KK | Katiba ya Kenya |
| KKA | Kamisheni ya Kitaifa ya Ardhi |
| KKUF | Kamati za kata za uhamishaji na fidia |
| KMUU | Kamati ya Utekelezaji wa Mpango wa uhamishwaj |
| KUFKN | Kamati za Uhamishaji na Fidia za Kaunti ndogo |
| KUM | Kitengo cha Usimamizi wa Mradi |
| KZ | Kaya Zilizoathirika |
| MK | Mazungumzo ya Kikundi |
| MKDN | Miundo ya Kinga Dhidi ya Mafuriko Nzoia |
| MKUMUHA | Mradi wa Kenya wa Uhakika wa Maji Ujasiri wa hali ya Anga |
| MSU | Mfumo wa Sera ya Uhamishwaji |
| MU | Mfereji unganishi |
| MULN | Mradi wa Umwagiliaji wa Lower Nzoia |
| MUM | Mpango wa Urejeshaji wa Maisha |
| MUU | Mpango wa Uhamishaji |
| MYK | Mashirika Ya Kijamii |
| MYS | Mashirika Yasiyo ya Serikali |
| NKK | Naibu Kamishna wa Kaunti |
| SMK | Shirika la Msitu Kenya |
| SO | Sera za Operesheni |
| SYU | Sera ya Uhamishaji |
| WANMM | Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Miji |
| WWM | Watu Walioathirika na Mradi |

# Orodha ya majedwali

Jedwali 1-1: Sehemu ya hatari za mpango wa utekelezi wa uhuamishwaji MUU wa III ……………….1-9

Jedwali 1-2: Jedwali la Mukhtasari wa wamiliki wa mali na mali zilizoathirika…………………………1-13

Jedwali 1-3: Ratiba ya makutani wa kijamii wa utambulisho na uhamasishaji………………………….1-15

Jedwali 1-4: Mikutano na machifu………………………………………………………………………1-17

Jedwali 1-5: Ratiba ya Mikutano na uongozi wa mtaa…………………………….……………………1-17

Jedwali 1-6: Athari za Mradi na hatua za upunguzaji……………………………………………………1-18

Jedwali 1-7: Ustahiki……………………………………………………………………………………....1-21

Jedwali 1-8: waliopoteza makao kabisa…………………………………………………………………..1-30

Jedwali 1-9: Muhtasari wa Mali zilizoathirika na gharama – Sehemu ya unyunyizaji…………….……1-31

Jedwali 1-10: Makadirio ya msaada wa urejeshaji hali za maisha……………………………………….1-33

Jedwali 1-11: Maelezo ya jumla yanayotoa muhtasari wa matokeo ya utafiti wa MUU………………..1-34

# 1 UFUPISHO

## 1.1 Utambulisho

### 1.1.1 Mamlaka ya Ripoti

Ripoti hii ya mwisho ya Mpango wa Utekelezaji wa Uhamishwaji (MUU) iliyopitiwa na kusasishwa imeandaliwa kwa kufuatia kifungu cha V (7) cha Masharti ya Kumbukumbu (MK) kwa Huduma za Ushauri na kusasisha Mpango wa Uhamishwaji (MUU) kwa Mradi wa Umwagiliaji wa Lower Nzoia (LNIP-I) na Miundo ya Kinga Dhidi ya Mafuriko Nzoia (MKDN) Zabuni No.MOWI/KWSCRP-1/006/2016-2017 ya tarehe 27 Machi mwaka wa elfu mbili kumi na saba (2017) kati ya **Wizara ya Maji na Umwagiliaji (MOWI)- Mradi wa Uhakika wa maji na Ustahimilivu wa hali ya Hewa nchini Kenya-Awamu ya Kwanza (KWSCRP-I) na Mshauri, GEDO Associates Ltd.**

Ripoti hii ni moja ya ripoti tatu za Mpango wa Utekelezaji Uhamishwaji (MUU) ambazo zimeandaliwa kulingana na pendekezo kutoka kwa Mteja.Ripoti hizo tatu tofauti zinahusu sehemu tofauti za mradi kama ifuatavyo:

- Ripoti ya Mpango wa Utekelezaji Uhamishwaji MUU I - Eneo la upokeaji la Nzoia hadi Mfereji mkuu
- Ripoti ya Mpango wa Utekelezaji Uhamishwaji MUU II - Daiki za Kusini na Kaskazini;
- Ripoti ya Mpango wa Utekelezaji Uhamishwaji MUU III - Ripoti Bloku 1 – 14 (Maeneo ya umwagiliaji).

Nakala ya barua-pepe inayoelekeza utengano wa ripoti hizo imewasilishwa katika kiambatisho 1.1
Ripoti hii ya mwisho imezingatia maoni yaliyopokewa kutoka kwa Mteja, Benki ya Dunia na KfW juu ya MUU 1 na 2 zilizosasishwa na Ripoti za Rasimu.Majibu ya maoni yametolewa katika kiambatisho 1.2 cha ripoti hii.

Ripoti hii ya mwisho imezingatia maoni yaliyopokewa kutoka kwa Mteja, Benki ya Dunia na KfW juu ya WWM 1 na 2 zilizosasishwa na Ripoti za Rasimu.Majibu ya maoni yametolewa katika kiambatisho 1.2 cha ripoti hii.

### 1.1.2 Asili ya Mradi

Kabla ya kuandaliwa kwa ripoti hii ya Mpango wa Utekelezaji Uhamishwaji (MUU), kulikuwa na Ripoti mbili za Mpango wa Uhamishwaji,moja kwa ajili ya mradi wa umwagiliaji wa Lower Nzoia iliyoandaliwa na Panafcon Ltd mwaka wa elfu mbili kumi na tatu (2013)na elfu mbili kumi na tano (2015) na nyingine kwa ajili ya daiki za Nzoia iliyoandaliwa na Tech Training and Research Ltd mwaka 2015. Ripoti hizo mbili zilitegemea hati za kina zilizoandaliwa na washauri tofauti.

**Sababu za kukagua na kusasisha ripoti hizo mbili ni:**

1. Uwezekano kwamba miundo ya miradi hiyo itabadilika kulingana na hatua ya ukaguzi wa muundo ambayo ingefanywa na mshauri wa utekelezaji kwa ajili ya mradi wa Umwagiliaji wa Lower Nzoia.Mshauri huyo alitarajiwa kufanya ukaguzi wa mwisho wa muundo huo na kutoa mapendekezo *(ukaguzi ulikamilishwa mwezi Juni mwaka wa elfu mbili kumi na saba (2017) na I na matokeo*

*yametumiwa katika utafiti wa Mpango huu wa Utekelezi wa Uhamishwaji).*

2. Ukweli ni kwamba zaidi ya miaka tatu (3) imepita tangu ripoti za Mpango wa Utekelezi wa Uhamishwaji zilipotayarishwa bila kutekelezwa,kwa maana ya kwamba hali ya msingi ya uchumi,sensa na thamani ya mali mwaka wa elfu mbili kumi ma tatu (2013) ingekuwa tofauti *(Tafiti mpya za sensa uchumi wa kijamii na hesabu ya mali na thamani iliyofanywa katika uchunguzi wa huu Mpango wa Utekelezi wa uhamishwaji MUU).*
3. Ripoti ya awali ya Mradi wa Umwagiliaji wa Lower Nzoia haikujumuisha mifereji ya umwagiliaji (sasa imejumuishwa).
4. Hitaji la uunganishaji wa mradi wa umwagiliaji wa lower nzoia na mradi wa daiki za Nzoia kuwa mradi mmoja na WWM moja kutokana na mwingiliano katika eneo la utekelezaji wa mradi na uwezekano wa watu waliaothirika na mradi (WWM) zizo hizo kujumuishwa katika maeneo yote mawili ya miradi (hii imeshughulikiwa katika ripoti hii).

Uhakiki na usasishaji wa Mipango ya Utekelezi wa Uhamishwaji ulihusu uthibitishaji na usasishaji wa sensa ya Watu walioathirika na mradi (WWM) walitambuliwa kulingana na tarehe ya awali,mali zilizoathirika,data ya msingi ya kiuchumi na kijamii ya watu walioathirika na mradi (WWM) ,wigo na ukubwa wa athari za kijamii zitakazobebwa na watu walioathirika na mradi (WWM) na muundo wa mpango sahihi wa uhamishwaji ambao utatoa usalama wa kijamii na hatua za fidia ili kurekebisha kikamilifu athari za uhamishwaji usio wa hiari kwenye maisha ya watu waliaothirika na mradi.

Uhakiki na kusasishwa kumetokana zaidi na miundo ya mwisho ya mradi wa umwagiliaji wa Lower Nzoia, na miundo ya kinga dhidi ya mafuriko ya Nzoia iliyoandaliwa na Washauri wa Utekelezaji (WU) wakiongozwa na  Lahmeyer International Consultants tarehe Juni mwaka wa elfu mbili kumi na saba (2017).

Uchunguzi wa sensa na hesabu ya mali kwa watu wote walioathirika na mradi (WWM) ulifanyika kuanzia tarehe 6 Mei-1 Agosti mwaka wa elfu mbili kumi na saba (2017) na Uchunguzi wa Kimsingi wa Uchumi wa Kijamii kutoka tarehe 5-19 Julai mwaka wa elfu mbili kumi na saba (2017) ndani ya maeneo yaliyoathirika kutoka eneo la upokeaji hadi mwisho wa mradi katika kata ndogo ya Mabinju katika fukwe za Ziwa Victoria.

## 1.2 Maelezo ya Mradi

### 1.2.1 Eneo la Umwagiliaji

Eneo la jumla la Mradi wa Umwagiliaji wa Lower Nzoia (LNIP-1) ni karibu hekta elfu tano mia nane (5,800) ukiondoa eneo la mabwawa na jumla ya eneo la umwagiliaji ni hekta elfu nne sabini na tano (4,075) zilizogawanywa kwa bloku 14 za umwagiliaji (Bloku 1-14). Mradi uliopo wa umwagiliaji wa Bunyala uliojengwa miaka ya sitini umejumuishwa ndani ya eneo la mradi na utafanyiwa ukarabati.

### 1.2.2 Sehemu ya Awamu ya kwanza ya Mradi wa Umwagiliaji wa Lower Nzoia

Awamu ya kwanza ya mradi umwagiliaji wa Lower Nzoia (LNIP-1) imetambuliwa kama uwekezaji wa kwanza utakaofadhiliwa chini ya Mradi wa Uhakika wa Maji na Ustahmilivu wa Hali ya Hewa (KWSCRP-I) utakaochangia matumizi ya maji yenye tija ambayo yanatumikia malengo ya ustahamilivu wa hali ya hewa.

**Shughuli za Mradi wa Umwagiliaji wa Lower Nzoia (LNIP 1) ni pamoja na:**

Ujenzi wa muundo wa upokeaji (bwawa dogo) na miundombinu inayohusika kuamuru uwezo uliotambuliwa katika kingo za kusini na kaskazini za mto Nzoia.Eneo la upokeaji (bwawa dogo) limependekezwa kwa kiwango cha kilomita 4 juu ya Daraja la Nzoia;

- Ujenzi wa usafirishaji,usambazaji maji na mifereji kwa eneo la umwagiliaji inalokadiriwa la hekta elfu saba mia sita tisini na saba (7,697) katika kingo zote za mto( Awamu 1- 4,075 ha katika kingo ya kushoto na Awamu ya 2-3,622 ha katika kingo ya upande wa kulia);
- Ukarabati wa miradi ya umwagiliaji ya Bunyala;
- Utoaji wa msaada wa kilimo na huduma za mnyororo wa thamani kwa wakulima wa mradi
- Uimarishaji wa uwezo wa kitaasisi wa utoaji wa huduma bora usimamizi wa miradi ya umwagiliaji kutoka Bodi ya kitaifa ya umwagiliaji / unyunyizaji na mashirika ya wakulima;
- Ujengaji uwezo wa wafanyakazi wa bodi ya kitaifa ya umwagiliaji / unyunyizaji ,wakulima na mashirika ya wakulima;
- Usimamizi wa mradi pamoja na utoaji wa Ufuatiliaji na tathmini, usalama wa mazingira na kijamii.

### 1.2.3 Sehemu ya Majengo ya Kinga Dhidi ya Mafuriko ya Nzoia

Majengo ya kinga dhidi ya mafuriko ya Nzoia inahusisha uboreshaji na uundaji mpya wa majengo ya kinga dhidi ya mafuriko yaliyopo, ambayo yanajumuisha daiki mbili-ya kusini na kaskazini-kila moja ikiwa kilomita kumi na saba (17). Daiki zilizopo zilijengwa miaka ya sabini (70) na wenyeji tangu wakati huo wamefanya makazi karibu na daiki hizo.

## 1.3 Wanufaika wa Mradi wa Lower Nzoia

Uwekezaji katika mradi wa umwagiliaji wa Lower Nzoia unatarajiwa kuwanufaisha moja kwa moja zaidi ya watu elfu ishirini (20,000), kaya elfu mbili mia moja (2,100), ikiwa ni pamoja na wakulima wadogo ambao kwa sasa wanafanya kilimo kinachosubiri mvua (haswa mahindi na maharage) na ufugaji.Watu wengine wanaokadiriwa elfu hamsini (50,000) wanatarajiwa kunufaika kupitia uhusiano katika shughuli za mradi na matokeo.Zaidi ya hayo, uchumi wa kaunti ndogo jirani utaimarishwa kwa kilimo cha umwagiliaji.

## 1.4 Malengo ya Mpango wa Utekelezi wa Uhamishwaji

Kulinga na Masharti ya Kumbukumbu (MK) kifungu cha saba (7), malengo ya mapitio ya MUU na usasishaji ni:

a) Kupitia na kusasisha MUU iliyopo ya mradi ili kuimarisha ufuataji wa sheria za serikali ya Kenya na sera, viwango na miongozo husika ya Benki ya Dunia. Haswa, kumbukumbu inapaswa kufanywa kwa sera ya operesheni ya Benki ya Dunia 4.12 kuhusu uhamishwaji usio wa hiari na pale ambapo

viwango vya benki hiyo vimethibitishwa kushikilia wigo mpana kuliko masharti ya kitaifa, viwango vya mwanzo vinatarajiwa kupewa kipaumbele na MUU inahitajika kutoa ipasavyo.

b) Kuhakikisha, kupitia, na kusasisha utafiti wa sensa ulofanywa kuhakikisha kuwa WMMs wote wanaofaa kulingana na tarehe na athari za uhamishwaji usio wa hiari zinatambuliwa na hatua muafaka za kupunguza athari za uhamishwaji na kulinda maisha zinapendekezwa

c) Kufanya utafiti wa kijamii na kiuchumi wa WWMs na kuhakikisha kuwa data za kimsingi zinatolewa kwa madhumuni ya ufuatiliaji na tathmini wakati wa kipindi cha utekelezaji wa mradi.

d) Kuhakikisha na kusasisha utafiti wa hesabu za mali na kuhakikisha kuwa mali zote ambazo zinaweza kuathiriwa na mradi huo pendekezi zinaorodheshwa, zinatiwa thamani na gharama.

e) Kuzinakili mali zote zilizothiriwa (mijengo, mazao, miti, ua) kwa kutumia Mfumo wa Vikao wa Tufeni (MVT) yenye usahihi wa mita 1 katika mfumo wa kodineti

f) Kuhakikisha ufuatiliaji wa sera za Benki ya Dunia za Uhamishwaji usio wa hiari na sheria nyingine zinzohusu uhamishaji na kanuni za makazi ambazo zinasimamia sekta ya maendeleo ya miundombinu

g) Kutoa miongozo/mikakati ya kuongeza ushiriki wa wadau na WMM katika michakato ya utambulisho, utekelezaji na ufuatiliaji ili kupunguza athari za uhamishaji za mradi. Miongozo itahusisha mfumowa usimamizi wa wadau (uchambuzi wa wadau na mpango wa mawasiliano,) kwa usimamizi wa shughuli za wadau kupitia mzunguko wa mradi

h) Kupendekeza hatua madhubuti za gharama nafuu na endelevu zitakazotekelezwa ili kurejesha na kuimarisha hali ya maisha ya watu walioathirika.

i) Kuandaa ripoti ya Mpango wa uhamishwaji (MUU) inayozingatia sheria za serikali ya Kenya na sera, viwango na miongozo ya Benki ya Dunia.

## 1.5 Wigo wa Mpango wa Utekelezaji uhamishwaji (MUU)

Kulingana na Masharti ya Kumbukumbu (MK) kifungu cha 7, malengo ya mapitio ya Mpango wa Utekelezi wa Uhamishwaji (MUU) na usasishaji ni: Maelezo ya Mradi;

- Maelezo ya Mradi;
- Kukagua na kusasisha muundo wa sheria;
- Sensa na utafiti wa kijamii na kiuchumi;
- Ushiriki wa umma,mashauriano na mawasiliano;
- Athari za mradi;
- Uthamini na fidia ya hasara;
- Uamuzi wa kustahiki;
- Mapendekezo ya hatua za uhamishwaji;
- Taratibu za kushughulikia malalamiko ;
- Mpangilio wa taasisi;
- Hatua za ufuatiliaji na tathmini;
- Utayarishaji wa Ratiba ya Utekelezaji

Ripoti za  zimeandaliwa kwa kuzingatia kanuni za mwongozo zilizoelezwa katika Mfumo wa Sera ya Uhamishwaji (MSU) ya mradi wa uhakika wa maji na ustahimilivu wa hali ya hewa kwa uhamishwaji usio wa hiari.Lengo kuu la MUU ni kupunguza athari mbaya kwa watu walioathirika na mradi (WWM) na kuboresha au angalau kurejesha masiha yao hadi viwango vya kabla ya mradi. MUU inajumuisha mpangilio wa taasisi,ratiba,bajeti ili kuwezesha ulipaji fidia na uhamishaji makazi mapya na mpango wa kushughulikia malalamiko ambao utafuatwa ili kushughulikia malalamiko/manung'uniko yatakayotokea kutokana na mradi huo.

## 1.6 Miundombinu ya mradi ambayo itaathiri mali na kusababisha watu kuondolewa kwenye makazi

Miundombinu ya umwagiliaji itahitaji upatikanaji wa eneo kubwa la ardhi ili kuwezesha utekelezaji wake.Eneo lililo chini ya Mradi wa utekelezi wa uhamishwaji MUU ni eneo la juu zaidi la mradi wa Lower Nzoia na linajumuisha yafuatayo:

**Jedwali 1-1: Sehemu ya hatari za mpango wa utekelezi wa uhuamishwaji MUU wa III**

| Eneo lililoathirika | Urefu (Kilomita) |
|---|---|
| Mfereji wa kwanza wa kwanza, MWK | 32 |
| Mfereji unganishi ya upili, MU6 | 2.4 |
| Mfereji unganishi ya upili, MU8 | 5.4 |
| Mfereji unganishi ya upili, MU9 | 4.6 |
| Mfereji unganishi ya upili, MU11 | 1.7 |
| Mfereji unganishi ya upili, MU12 | 4.5 |
| Mfereji unganishi ya upili, MU13 | 4.2 |
| Mfereji unganishi ya upili, MU14 | 6.8 |
| Main Drain 1, MD1 | 10.1 |
| Main Drain 2, MD2 | 11 |
| **Urefu** | **82.7** |

## 1.7 Utafiti wa Kijamii na Kiuchumi na Matokeo

### 1.7.1 Utafiti wa Kijamii na Kiuchumi

Utafiti ulifanywa kati ya tarehe 6 – 1 Agosti mwaka wa elfu mbili kumi na saba (2017) kwa mradi wote kuanzia eneo la MUU III kwa kutumia vikaratasi vya maswali ambavyo vilihusisha maswali yaliyogawanywa sehemu tatu kuhusu tabia za kaya, shughuli za kiuchumi, huduma za kijamii ikiwa ni pamoja na miundombinu, elimu, tabia za kiafya, umiliki wa ardhi na matumizi na mlengwa Ushiriki.  Utafiti wa kijamii na kiuchumi uliwahoji watu mia saba sitini na mmoja (761) kati ya idadi ya watu elfu tatu mia mbili ishirini na tisa (3,229) walioathirika na mradi WWM katika ushoroba wa mradi, ambao ni takriban asilimia thelathini (30%)

### 1.7.2 Matokeo ya Utafiti wa Kijamii na Kiuchumi

Baadhi ya matokeo ya utafiti wa kijamii na kiuchumi ni kama yafuatayo:

- Eneo la MUU liko katika kauti za Siaya na Busia. Makadirio za watu ni 81,920 (Wanaume elfu thelathini na nane,mia tisa sitini na mbili (38,962) na Wanawake elfu arubaini na mbili mia tisa hamsini na nane (42,958) na makadirio ya idadi ya watu kutoka sensa ya mwaka elfu mbili na tisa (2009 );
- Eneo lina huduma za kijamii za kati ya wastani na nzuri na miundombinu ikiwa ni pamoja na barabara, usalama, mawasiliano, nishati, vituo vya masoko, n.k;

- Viwango vya umaskini vimechukuliwa kama vya County ya Busia, ambavyo ni karibu asilimia sitini na nne nukta mbili (64.2%) (Mpango wa Maendeleo wa Kaunti 2013 - 2017) na juu zaidi kuliko wastani wa kitaifa wa asilimia arubaini na tano nukta tisa (45.9) na hivyo kuchukuliwa kuwa juu;
- Sababu za umaskini katika maeneo haya ni nyingi na tofauti na ni pamoja na udongo ulikosa rotuba unaochangia mazao kidogo, kipato cha chini katika kaya kuweza kununua pembejeo, kutegemea sanaa mbinu za zamani za kilimo na kukosa vyanzo mbadala vya mapato;
- Utafiti huo ulibaini kuwa baadhi ya kaya zilikuwa na zaidi ya mtu mmoja aliye katika mazingira magumu ikiwa ni pamoja wazee zaidi ya miaka sitini na tano (65) – 30.3%), watu walio na ulemavu unaoonekana au ulemavu wa akili asilimia kumi nukta nane (10.8%), mayatima asilimia kumi ta tano nukta saba (15.7%), walio na maradhi sugu asilimia saba nukta tisa (7.9%) na VVU/Ukimwi asilimia kumi nukta nne (10.4%);
- Ilinakiliwa kuwa kaya zilizoathirika zinahusisha viongozi wa kaya wanawake ambao wanafikia asilimia thelathini na tano (35%) ya waliohojiwa. Hawa ni pamoja na wajane ambao wanaunda kundi kubwa katika vingozi wa kaya wanawake ilhali wengine wameachika au hawajaolewa. Wajane wanachukuliwa kama watu walio kwenye mazingira magumu na watahitaji uangalifu maalum.
- Wastani wa idadi ya watu katika eneo hilo wamesoma huku wengi wao wakiwa wamepata elimu ya shule ya msingi na zaidi na ilikuwa wazi kutoka kwenye mikutano kuwa wana uwezo wa kuhoji habari zinazotolewa na pia jinsi inavyoathiri na kuhudumia watu na hii inaweza kuhusishwa na kiwango cha elimu.
- Kuna kituo cha afya katika kila kata ndogo kilichoko karibu (< kilomita mbili). Ugonjwa wa kawaida ni malaria asilimia tisini na nne nukta moja (94.1%) ikufuatiwa na magonjwa yanayotokana na maji asilimia ishirini na sita nukta moja (26.1%) ikiwa ni pamoja na kuharisha, homa ya matumbo (typhoid), kipindupindu na amoeba ikitoa wito wa kuchukuliwa hatua za kuhakikisha utibuji wa maji pamoja na uboreshaji wa usafi wa mazingira.
- VVU/Ukimwi uko asilimia kumi na saba (17%) na ni changamoto kubwa kwa sababu uko juu kuliko maambukizi ya kitaifa ya asilimia sita nukta mbili (6.2%) (kiwango katika kaunti ya Busia na Siaya ni asilimia saba nukta nne (7.4%) na asilimia kumi na saba nukta nane (17.8%). HIV/Ukimwi unaongeza mzigo katika uchumi wa kaya na watoaji huduma za afya. Katika mchakato wa MUU walioathirika watahitaji msaada maalum iwapo watahama ili kuhakikisha wanaendelea kupata utunzaji, na matibabu.

- Kuna lishe duni katika eneo hilo na kuna mpango wa kujitolea wa afya ya jamii/kamati za afya kwa ushirikiano na AMREF ambao unatoa chakula/virutubisho vya lishe kwa watoto walioathirika. Kulingana na ripoti ya hivi karibuni ya KDHS (2008- 09), asilimia thelathini na nne (34%) ya watoto walio chini ya umri wa miaka tano (5) katika ukanda wa magharibi, ikiwa ni pamoja na Siaya wanakosa chakula kutokana na umaskini haswa kwa watoto.

- Katika utafiti huo ilibainika kuwa wale wanaopata maji safi wanayachota pengine kutoka kwa kisima, mabomba ya maji au matanki na wanajumuisha asilimia sitini na moja nukta saba (61.7%) (msimu wa mvua) na asilimia arobaini na nne nukta nne (44.4%) (msimu wa ukame). Wengine wanatumia maji yaliyoko nje kwenye vidimbwi ambayo sio salama kwa matumizi ya nyumbani na hii huenda ikawa sababu ya magonjwa yanayotokana na maji.

- Kama asilimia saba nukta tisa (7.9%) ya kaya hazina uwezo wa kupata vyoo na kuna kinyesi kimetapakaa kila mahali na hii ni hatari kwa afya ambayo inaathiri jamii yote. Aina ya kawaida ya choo katika viwango vya kaya ni choo cha shimo ikiwa asilimia themanini na nane nukta sita 88.6%.

- Umiliki wa ardhi-ardhi inamilikiwa kibinafsi na takriban asilimia themanini na nane nukta sita (88.6%) ya ardhi imerithiwa na idadi kubwa ya vyeti vya umiliki wa ardhi bado viko katika majina ya waliofariki, ubadilishaji wa umiliki haujafanywa na watu wengi asilimia themanini na tano nukta mbili (85.2%) hawajachukua hatua ya kusajili ardhi zao na walalamika kwamba gharama za usajili ni ghali mno. Ukubwa wa ardhi ni wastani wa ekar moja hadi mbili (1-2)na hata ndogo zaidi kutokana na mgawanyo mdogo.

- Katika hali nyingi ardhi inatumika kwa makazi, kilimo cha mazao na ufugaji. Kilimo cha mazo/kilimo kiko katika kiwango cha matumizi ya nyumbani. Mazao yote ya chakula na biashara yanapandwa.

- Umiliki wa Ardhi - Kimsingi jamii ni za kizalendo na kwa hivyo wanaume ambao wanamiliki ardhi na urithi wa aina yoyote wa mali hufafanuliwa wazi kwenye safu za kiume za kizazi. Kutoka msimamo w akitamaduni mwanamke hamiliki ardhi na hawezi kurithi ardhi hata kama mumewe akifariki;

- Kuna wajane mia tano kumi na tisa (519) walioathirika na mradi ambao huenda wakanyimwa haki zao wakati wa MUU kama ilivyosisitizwa wakati wa Mazungumzo ya Kikundi (MK).Katika kupunguza athari, hawa watapatiwa kipaumbele na umaalum wakati wa ugawaji wa ardhi na michakato ya fidia.;

- Chanzo kikuu cha mapato kwa wengi waliohojiwa asilimia themanini na saba nukta moja (87.1%) ni kilimo cha mazao, ambacho kwa kawaida hufanywa kwa kutegemea mvua, ambayo wakati mwingine inakuwa chache na isiyotegemewa. Matumizi ya mbegu zilizothibitishwa, mbolea na

pembejeo ni nadra. Uzalishaji wa mazao hata hivyo unatarajiwa kuboreka kutokana na kuanzishwa kwa umwagiliaji na mbinu mpya za kilimo;

- Vyanzo vingine vya mapato ni pamoja na mifugo, ufugaji samaki, ajira rasmi na zisizo rasmi, biashara, malipo ya uzeeni n.k
- Mapato ya kaya ni wastani wa shilingi elfu kumi na nne mia tano tisini na mbili (Ksh.14,592) kwa mwezi (dola za marekani mia moja arubaini na mbili (142) kwa mwezi au dola za marekani nne nukta saba (4.7) kwa siku na haswa kutoka kwa wale walio kwenye ajira rasmi, biashara na vibarua;
- Kuna ukosefu wa chakula katika viwango vya kaya kwa sababu wakulima wanashindwa kuzalisha chakula cha kutosha chini ya mazingira ya kutegemea mvua kutokana na mabadiliko ya hali ya anga yasiyotabirika na kulingana na mahojiano gharama za kaya nyingi ziko juu kwa chakula kwa sababu mavuno ni kidogo na hayatoshi kukidhi mahitaji ya uhakika wa chakula ya kaya. Kilimo bora cha umwagiliaji kitaongeza uzalishaji wa chakula.
- Uchambuzi wa kijinsia - Wanawake wanapata mali ya kifamilia na hufanya majukumu ya usimamizi bila udhibiti wa mapato na wanaume wana nguvu ya kufanya maamuzi na wanamiliki pamoja kudhibiti ardhi ambayo ni rasilimali kuu chini ya huu mradi na pia ni muhimu chini ya mchakato wa MUU.Kwa kitamaduni wanawake hawadai umiliki wa ardhi lakini wanaweza kuitumia kwa kwa uzalishaji wa chakula.Wanawake hawadai umiliki wa ardhi ndani ya familia na vijana wa kiume wanweza kumiliki ardhi tu wakati wameanzisha familia zao.;
- Viwango vya ufahamu wa mradi katika ngazi ya kaya l - Kutoka kwa mahojiano na mazungumzo ya vikundi, iliibuka kuwa asilimia tisini na nane nukta nne (98.4%) ya waliohojiwa walikuwa na ufahamu kuhusu mradi uliopendekezwa wa Mradi wa Umwagiliaji wa Lower Nzoia (MULN) na zaidi ya asilimia tisini nukta nane (90.8%) wanauunga mkono;
- Faida chanya za mradi - Zaidi ya 80% ilionyesha kuwa mradi utatoa maji kwa ajili ya umwagiliaji na matumizi ya nyumbani, kilimo kilichoboreshwa, uhakika wa chakula, na matumizi ya ardhi ya kiwango cha juu ambayo inahitajika;
- Athari hasi za mradi - Waliohojiwa walieleza kuwa mradi utakuwa na athari hasi kama vile mgawanyo/upoteaji wa ardhi na/au mali, uhamishwaji/upotezaji wa nyumba,ukataji miti na uingiliaji wa mfumo wa ikolojia,hatari/magonjwa,kelele na uharibifu wa udongo, miongoni mwa mambo mengine. Walitoa maoni ya kuzuia athari mbaya na haya yanawasilishwa katika Kifungu 7.2.12 cha hii Ripoti;
- Wale waliotharika na mradi walionyesha wasiwasi na kupendekeza hatua ambazo zitawalinda kutokana na athari za mradi
- Watu walioathirika na mradi wanaohitaji kuhamishwa hawatataka kuhamishwa mbali na wanapoishi sasa.
- Watu walioathirika wanapaswa kulipwa fidia ya kutosha na kupewa muda wa kuhama.
- Hatua zinafaa kuwekwa kuwasaidia wakulima kuuza mazao yao.
- Mradi umechukua muda mrefu kutekelezwa. Jamii inayoishi eneo la mradi inasubiri kuvuna faida za mradi;

## 1.8 Utafiti wa sensa na Matokeo

### 1.8.1 Utafiti wa sensa/Utafiti

Utafiti wa sensa ulifanywa ndani ya eneo la MUU III kwa kuanzia eneo la uunganishaji na mifereji kutoka tarehe 8 -14 Mei mwaka wa elfu mbili kumi na saba (2017), na sehemu ya mtiririko wa nyuma kutoka tarehe

6 Mai – 1 Agosti mwaka wa elfu mbili kumi na saba (2017). Sensa ilifanywa kwa ushirikiano na utawala wa eneo la mradi na jamii zilizoathirika na majadiliano mengi yalifanyika

Sensa ilihusisha utembeaji kwenye eneo na mahojiano katika kila nyumba na kaya ambayo ilipatikana ndani ya miundombinu ya mradi inatoa nafasi ya kuwatafuta wenyewe na ukubwa wa ardhi iliyoathirika, aina na ukubwa wa mijengo iliyoathirika, mazao, na mali maalum kama vile makaburi pamoja na biashara zilizoathirika.

Data za sensa za kila kaya iliyoathirika zilikusanywa kwa kutumia vikaratasi vya maswali yanayohusu umiliki wa ardhi pamoja na uthibitishaji wa hati za umiliki ,data ya idadi ya kaya,mali zilizoathirika na mijengo mingine,upendeleo wa fidia,makundi yaliyo kwenye mazingira magumu k.m wasiojiweza,wajane na wazee,mayatima na watoto walio kwenye mazingira magumu ,kaya zinazoongozwa na wanawake na vipengele vya kitamaduni, miongoni mwa mambo megine kwa kutumia kifaa cha sensa.Zaidi ya hayo, utambulisho na hesabu ya mali za jamii na taasisi na miundombinu, za kibinafsi na umma ,ziliandikishwa kwa madhumuni ya fidia,na/au uhamishwaji.

### 1.8.2 Matokeo ya Sensa

Data zilizokusanywa kutoka nyanjani ilichambuliwa na yafuatayo yameanzishwa, miongoni mwa mengine:

- Watu walioathirika na mradi (WWMs);
- Jumla ya ardhi iliyoathirika;
- Nambari za sehemu zilizoathirika;
- Maliasili zilizoathirika;
- Utambuaji wa watu walio kwenye mazingira magumu k.m wasiojiweza, wajane, wazee, mayatima na watoto walio kwenye mazingira magumumiongoni mwa wengine.
- Maelezo ya mijengo iliyoathirika na mali zingine;
- Upendeleo wa fidia.
- Data ya sensa iliyochambuliwa

Kutoka kwa sensa, idadi ya watu walioathirika na mradi WWM wamiliki wa mali na mali zinazohusiana nazo ambazo zimeathirika zimeanzishwa na hii imefupishwa katika jedwali 1-2.

Data ya sensa iliyochambuliwa imewasilishwa katika kiambatisho C cha ripoti hii.
Kutoka kwenye jedwali, idadi ya watu walioathirika na mradi WWMs/idadi ya wamiliki wa mali ni elfu tatu mia mbili ishirini na tisa (3,229). Idadi ya watu walioathirika na mradi ni elfu kumi na mbili mia tano sitini na moja (12,561) ambapo kati ya hao kuna watu elfu tatu mia nne hamsini na moja (3,451) walio kwenye mazingira magumu katika kaya 1,283.

Mali zilizoathirika ni pamoja na ardhi, mijengo, miti na mazao na mali maalum (makaburi). Hakuna biashara na ardhi ya umma iliyoathirika kama inavyooneshwa kwenye meza. Eneo la ardhi iliyoathirika ni hekta mia

moja tisini na sita (196) (ekari 486) na kuna watu walioathirika mia tatu thelathini na nane (338) wanaopoteza ardhi na pia mijengo.

**Jedwali 1-2:** Sehemu ya hatari za Mpango wa Utekelezi wa Uhamishwaji MUU III

| **#** | **Vitu** | | | **Idadi** |
|---|---|---|---|---|
| A | Idadi ya walioathirika | | | |
| | Jumla ya idadi wa wamiliki wa mali walioathirika (watu binafsi,Kaya na Taasisi) | | | 3,229 |
| | | **Jumla** | | **943** |
| | Idadi ya walioathirika na mradi (WWMs) | Watu wazima | Wanaume | 3,816 |
| | | | Wanawake | 2,806 |
| | | Watoto | Wanaume | 1,790 |
| | | | Wanawake | 1,600 |
| | | Hawajaainishwa (Watu wazima au watoto) | Wanaume | 959 |
| | | | Wanawake | 419 |
| | | Jinsia ambayo haijabainishwa | | 1,171 |
| | Makundi ya watu wenye mazingira magumu | **Kaya zilizoathirika** | | **1,283** |
| | | Wazee | | 655 |
| | | Wenye matatizo ya akili | | 187 |
| | | Mayatima | | 418 |
| | | Wasiojiweza | | 428 |
| | | Magonjwa mahututi au wagonjwa (Pumu,Kifafa, Anemia selimundu, | | 567 |
| | | Magonjwa ( Ukimwi) | | 677 |
| | | Wajane | | 519 |
| **B** | **Waathirika waliokosa kabisa** | | | 105 |
| **C** | **Ardhi iliyoathirika** | | | |
| | Jumla ya idadi ya vipande vya ardhi vilivyoathirika | | | 2,807 |
| | Vipande vya ardhi vinavyomilikiwa na watu binafsi | | | 2,788 |
| | Shule/Vyuo | | | 7 |
| | Serikali za Kaunti | | | 3 |
| | Makanisa | | | 8 |
| | Ardhi ya jamii | | | 1 |
| | Jumla ya ukubwa wa ardhi itakayochukuliwa kwa ajili ya mradi wa mradi wa umwagiliaji wa Lower Nzoia Awamu ya 2 | | | **196 hecta/ 486 acres** |

| | | |
|---|---|---|
| **D** | **Mijengo iliyoathirika** | |
| | Jumla ya idadi ya mijengo ya kaya iliyoathirika | 697 |
| | Jumla ya idadi ya mijengo iliyoathirika | 1,382 |
| **E** | **Miti na mazao yaliyoathirika** | |
| | Idadi kamili ya kaya zilizo na miti zilizoathirika | 967 |
| | Miti kwa ajili ya bidhaa za mbao (Mkangazi, mkaratusi, mpaina,mti grevilia,Mvinje, Ober', 'Ciala, n.k) na miti ya matunda (Maembe, Parachichi, mapera, Paipai, n.k') | 44,431 |
| | Idadi kamili ya kaya zilizo na mazao yaliyoathirika | 71 |
| | Idadi kamili ya mazao yaliyoathirika | Mazao mbalimbali |
| **F** | Biashara zilizoathirika | |
| | Idadi kamili ya kaya zenya biashara zilizoathirika | 49 |
| | Idadi ya biashara zilizoathirika | 56 |
| **G** | **Makaburi** | |
| | Idadi kamili ya kaya zenye makaburi yaliyoathirika | **181** |
| | Idadi kamili ya makaburi yaliyoathirika | **546** |

Watu walio kwenye mazingira magumu walioathirika na mradi ni watu ambao kwa sababu ya jinsia, mazoea ya kitamaduni,umri,ulemavu wa mwili au akili,shida za kiuchumi au hadhi ya kijamii inaweza kuathiriwa vibaya na uhamishwaji kuliko wengine ambao wanaweza kuwa na uwezo mdogo wa kudai au kuchukua fursa ya usaidizi wa uhamishwaji na faida zinazohusiana.Inahitajika kuweka idadi yao vizuri ili kuhakikisha kuwa wakati wa fidia wanawakilishwa na shida zao hazipuuzwi.Kamati ya kushughulikia malalamiko itahakikisha kwa makusudi malalamiko yao yanawakilishwa kwa usawa wakati wa fidia.

Kaya zenye mazingira magumu zinastahili msaada wa mpito wa Shilingi elfu mia moja (Ksh. 100,000) kwa kila kaya chini ya MUU kwa sababu zina mahitaji maalum. Kiwango hicho kitashughulikia matayarisho ya ardhi, mafunzo na mkopo, ushauri nasaha, matunzo ya kijamii na kujenga mitandao ya kijamii kwa ajili ya walio kwenye hatari.Zaidi ya hayo, wajane watahitaji msaada zaidi katika suala la urithi wa ardhi kuhakikisha kuwa hawatanyang'anywa ardhi zao.

## 1.9 Mikutano ya Mashauriano ya wadau na watu waliyoathirika na mradi (WWMs)

Mikutano ya Mashauriano kati ya wadau na watu walioathirika na mradi ilifanyika katika eneo la mradi kutoka tarehe 27 Aprili hadi tarehe 9 Juni mwaka wa elfu mbili kumi na saba (2017). Mikutano ya Mashauriano ya wadau na walioathirika yaliusisha yafuatayo:

- Wito wa hisani na mikutano ya utambulisho katika ofisi za kaunti na kaunti ndogo;
- Mkutano wa wadau na utawala wa mitaa na viongozi;
- Mikutano ya kijamii ya utambulisho na uhamasishaji;
- Mikutano ya maendeleo na machifu wa kata katika eneo;
- Mikutano ya mashauriano na watu walioathirika na mradi (WWMs) kwa uanzishaji wa kamati za kata ndogo na kata za fidia.

Muhtasari wa hayo hapo juu unawasilishwa hapa chini:

### 1.9.1 Wito wa hisani

Mkutano wa Wito wa hisani ulifanywa katika kaunti za Siaya na Busia tarehe 25 na 26 Aprili mtawaliwa katika hatua za mwanzo. Wakati wa Mkutano huo wa hisani, mteja alitoa muhtasari wa asili ya mradi wa umwagiliaji wa Lower Nzoia (MULN) na mijengo ya kuzuia mafuriko ya Nzoia halafu akaitambulisha kampuni ya GEDO Associates Ltd, mshauri wa MUU aliyetwikwa jukumu la kupitia na kusasisha Mipango ya Uhamishwaji kwa ajili ya umwagiliaji na mfumo wa maji na mijengo ya kuzuia mafuriko ya Nzoia.Maelezo ya mkutano huo yaliwasilishwa katika Ripoti ya mwanzo ya Mei mwaka wa elfu mbili kumi na saba (2017).

### 1.9.2 Mkutano wa wadau na viongozi na utawala wa mitaa

Mkutano wa wadau kwa eneo lote la mradi ulifanyika tarehe 27 Aprili mwaka wa elfu mbili kumi na saba (2017) katika kituo cha Uranga Good Samaritan Centre pamoja na utawala wa mitaa (Naibu Kamishna wa Kaunti,machifu na manaibu wa chifu)na wawakilishi wa wakulima.Mkutano huu ulikuwa muhimu kwa mteja,kama alivyowakilishwa na Ms Nyawira wa bodi ya kitaifa ya umwagiliaji / unyunyizaji,kuitambulisha timu ya Mshauri.Viongozi walikubaliana na kujitolea kushiriki katika mchakato wa MUU na mpango wa uhamasishaji wa jamii uliandikwa.Viongozi waliendesha uhamasishaji na mikutano iliandaliwa kulingana na ratiba.

### 1.9.3 Mikutano ya kijamii ya utambulisho na uhamasishaji

Mikutano ya kijamii ya utangulizi na uhamasishaji ilifanyika katika maeneo ya unyunyuzi. Wakati wa mikutano ya utambulisho, timu ya mshauri wa MUU ilitambulishwa na mwenyeji utawala wa mitaa baada ya hapo mshauri akatoa muhtasari wa asili ya mradi na kuwaeleza waliohudhuria kwamba GEDO Associates Ltd imepewa kazi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kufanya upitiaji na usasishaji wa Mipango ya Uhamishwaji kwa ajili ya mradi wa umwagiliaji wa Lower Nzoia (MULN) na Mijengo ya Kukinga Mafuriko ya Nzoia (MKDN) iliyoandaliwa kati ya mwaka elfu mbili kumi na tatu hadi elfu mbili kumi na tano (2013 – 2015).

- Uamuzi na ununuzi wa ukanda wa mfereji ,katika kingo za kulia na kushoto unaojulikana kama (sehemu ya umwagiliaji ya kusini na kaskazini , mtawalia )
- Uchunguzi na uekaji alama wa Miundombinu
- Utambuaji wa watu waliaothirika na sensa ya mradi na utafiti wa kimsingi wa kiuchumi na kijamii wa watu walioathirika na mradi WWM;
- Uthamini wa mali zilizoathirika
- Mikutano ya uhamasishaji ya WWM;
- Uundaji wa kamati za malalamiko na utatuzi wa migogoro

Mshauri alisisitiza umuhimu wa jamii kushirikiana na timu ya mshauri, wanaofanya hesabu, viongozi wa mitaa na wawakilishi wa wakulima wakati wa ukusanyaji wa data. Zaidi ya hayo, jamii ilielezwa kuhusu umbali ya maeneo ya unyunyuzi na kwamba mwanzo wake utakuwa katika sehemu/block 1-sehemu/bloku 14 (Angalia kumbukumbu za mahudhurio katika kiambhishi 3)

**Jedwali 1-1: Ratiba ya makutani wa kijamii wa utambulisho na uhamasishaji**

| Tarehe ya Mkutano | Ukumbi wa mkutano | Bloku | Lengo | Waliohudhuria | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Wanaume | Wanawake |
| 3/5/2017 | Ofisi kuu ya Unyunyizaji wa Bunyala | Bloku 7,8 & 9 | Utambulisho wa mradi wa umwagiliaji na kuwaalika walioko unyunyuzi kushiriki kikamilifu katika mradi | 87 | 37 |
| 4/5/2017 | Eneo la Baraza la Chifu wa Manga | Bloku 5 | | 33 | 51 |
| 5/5/2017 | Soko la Nzoia | Bloku 1 | | 41 | 35 |
| | Uwanja wa Zahanati wa Rabar | Bloku 2 & 3 | | 67 | 46 |
| | Musengese Center / Church of God Grounds (Uwanja wa Kanisa la Musengese) | Bloku 11, 12, 13 & 14 | | 60 | 35 |
| 9/5/2017 | Soko la Nyabera | Bloku 4 | | 57 | 52 |
| 10/5/2017 | Soko la Mubwayo / Posta | Bloku 10 | | 105 | 25 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 11/5/2017 | Ofisi ya Naibu Chifu Nyadorera | Bloku 6 | | 44 | 27 |

### 1.9.4 Mkutano wa maendeleo na machifu wa kata

Mikutano zaidi iliandaliwa na machifu~~. Haya~~ haya yalikuwa mashauriano kuhusu maendeleo ya kazi na pia kushiriki katika majadiliano ya kina kuhusu masuala ya kiuchumi, kijamii na kitamaduni. Mitano kati ya mikutano hiyo ilifanywa katika maeneo ya mpango wa uhamishwaji MUU III kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali 1-4 hapo chini.

**Jedwali 1-2: Mikutano na machifu**

| Tarehe | Ukumbi | Ukumbi na bloku |
|---|---|---|
| 7/6/2017 | Afisi ya Chifu Mwer | Kusini Magharibi wa Alego bloku 5 |
| 8/6/2017 | Afisi ya Chifu Uranga | Alego magaribi bloku 2,3 na 4 |
| 8/6/2017 | Afisi ya Chifu Harambee | Usonga - blocku 6,sehemu ya bloku 7, sehemu ya block 10 na sehemu ya bloku 11 |
| 9/6/2017 | Afisi ya Chifu Mau Mau | Bunyala ya kati iliyoshika Sehemu ya bloku 7, bloku 8 na sehemu kidogo ya bloku 10 |
| 9/6/2017 | Afisi ya Chifu Musoma Beach | Khajula sehemu ya bloku 10, sehemu ya bloku 11, bloku 12,13 na 14 |

### 1.9.5 Mkutano wa mashauriano kwa ajili ya kuanzisha uhamishaji wa kata na kata ndogo Kamati za fidia.

Mikutano ya ziada ilifanyika mwezi Julai pamoja na WWMs katika ngazi za kata na kata ndogo ambayo ilipelekea uundwaji wa kamati za uhamishaji na fidia ndani ya sehemu ya MUU. Kamati hizo zitashughulikia malalamiko na migogoro inayohusiana na uhamishwaji na fidia. Wanachama wa kamati walichaguliwa kutoka miongoni mwa watu walioathirika na mradi WWMs. Ratiba ya mikutano imeonyeshwa kwenye jedwali 1-5.

**Jedwali 1-3: Ratiba ya Mikutano na uongozi wa mtaa**

| Tarehe | Eneo la utawala | Ukumbi |
|---|---|---|
| Julai 19, 2017 | Bunyala wa kati – Khajula | Uwanja wa bodi ya kitaifa ya umwagiliaji / unyunyizaji |
| Julai20, 2017 | Usonga<br>Kusini magaribi wa Alego | Soko la Sidundo<br>Uwanja wa Manga |
| Julai 21, 2017 | Alego magaribi<br>Umala na Ambira | Uwanja wa zahanati ya Rabar |

## 1.10 Tarehe ya Mwisho

Tarehe ya mwisho iliwekwa kuwa tarehe 3 Mei mwaka wa elfu mbili kumi na saba (2017) na ilitangazwa kwa watu walioathirika na mradi WWMs wakati wa mikutano ya mashauriano na tarehe hiyo ilipitishwa rasmi na walioathirika wote.Tarehe hiyo iliweka makataa ya ustahiki wa fidia kwa wanaofaa na walioorodheshwa kwa sababu mradi wa umwagiliaji wa Lower Nzoia na mijengo ya kinga dhidi ya mafuriko ni kutafuta ardhi ,mali,miti,mazao,na mijengo iliyoko ndani ya eneo la miundombinu ya mradi.Maendeleo mengine mapya au mijengo iliyojengwa na walioathirika katika ukanda wa miundombinu ya mradi baada ya tarehe ya mwisho hawastahiki kuhamishwa au kulipwa fidia. Hii ni kwa sababu shughuli hii ilikuwa usasishaji wa MMU ambayo ilifanyika mwaka wa elfu mbili kumi na tatu (2013) na mwaka wa elfu mbili kumi na tano (2015) na ndio sababu ilifanywa mwanzoni mwa sensa.

## 1.11 Sera ya uhamishaji na haki stahiki

Utafiti ulifanywa kulingana na sheria husika za Sheria za Ardhi mwaka wa elfu mbili kumi na mbili (2012), Sheria ya Usajili wa Ardhi mwaka wa elfu mbili kumi na mbili (2012), Sheria ya Kitaifa ya Tume ya Ardhi 2012, pamoja na sera ya uhamishwaji usio wa hiari ya Benki ya Dunia (Sera za Operesheni 4.12), miongoni mwa nyingine, kama ilivyoonyeshwa katika kifungu cha (tano) 5 cha ripoti hii.

Muswada wa uhamishaji na makazi umepelekwa kwa mwanasheria mkuu kwa ajili ya kuchapishwa. Muswada huo unazungumzia ufukuzwaji usio wa hiari, fidia na uhamishwaji. Sheria za ardhi za Kenya na katiba ya Kenya (KK) inapendekeza kuwe na fidia ya haki kwa walioathirika lakini haikufafanua wazi kuhusu ni kipi kinaweza kuwa fidia ya haki. Benki ya Dunia OP.4.12 inapendekeza gharama zote mbadala za ardhi na mijengo katikaviwango vya sasa vya soko.

**Sera za usalama unaohusiana na uhamishwaji na makazi mapya za Benki ya Dunia**

Sera husika za Benki ya Dunia pia zimepitiwa. Mradi umetathminiwa na mazingatio kufanywa kuhusu jinsi sheria na sera zinasababishwa.

**Uhamishwaji usio wa hiari: Sera za Operesheni 4.12**

Sera ya uendeshaji ya Benki ya Dunia 4.12: uhamishwaji usio wa hiari umesbabishwa na mradi kwa kuwa mradi wa umwagiliaji na mijengo ya kinga dhidi ya mafuriko yatachukua ardhi, athiri nyumba za kuishi, mijengo mingine na miti.

## 1.12 Wasiwasi wa Watu Waliotharika na Mradi (WWM)

Wakati wa sensa na utafiti wa kiuchumi na kijamii, watu walioathirika na mradi (WWM) walikuwa na wasiwasi kwamba miundombinu ya mradi wa umwagiliaji itaathiri mahusiano ya kijamii na mwingiliano.Shughuli za mradi zitaathiri kwa kiwango fulani,mawasiliano miongoni mwa walioathirika kutokana na miundombinu ya mifereji.

Kunaweza kuwa na harakati kidogo ndani ya jamii na kati ya jamii na ufikiaji wa huduma za kijamii na umma. Ufikiaji mto wa Nzoia ambao ni chanzo cha maji kwa matumizi ya nyumbani na pia samaki na mifugo, utazuiwa.

Hata hivyo, kupunguza athari hizi, muundo wa mradi umejumuisha njia za miguu, madaraja na ngazi kuhakikisha ufikiaji rahisi kati ya sehemu zilizoathirika na jamii pamoja na ufikiaji wa maji kwa kaya zilizoathirika, na pia mifugo. Vituo vya maji kwa ajili ya wanyama wanaofugwa vimewekwa pembezoni mwa mifereji.

## 1.13 Muhutasari wa athari za mradi na hatua za kukabiliana nazo

Kama ilivyoelezwa tayari, shughuli za mradi zitaleta athari ambazo zinaweza kukabiliwa. Muhtasari wa athari zinazotarajiwa na hatua za kukabiliana nazo zimeelezwa katika Meza 1-9 na ni pamoja na yafuatayo.

- Upotezaji wa ardhi;
- Upotezaji wa mazao;
- Upotezaji wa miti;
- Upotezaji wa mijengo ya kuishi;
- Athari kwenye makaburi.
- Athari kwa watu walio kwenye mazingira magumu

Ripoti hii inapendekeza fidia ya upotezaji wa mali zote hapo juu kwa kiwango cha gharama kamili za mbadala.

**Jedwali 1-4 Athari za Mradi na hatua za upunguzaji**

| | Idadi ya watu walioathirika | Mali zilizoathirika | Athari | Uzuiaji |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Watu binafsi wanaoishi ndani ya ukanda wa mradi | Nyumba za kuishi, Huduma za choo na mijengo mingine | 12,561 WWMs( 6,565 Wanaume, 4,825 Wanawake na 1,171 Waliokosa kujitambilisha | ~ uhamasishaji<br>~ Fidia na uhamishwaji |
| 2 | ~ Watu binafsi walio na ardhi karibu<br>~ Watoto na wafanyi kazi za mashule<br>~ Wanakijiji wa makanisa mbalimbali,<br>~ Wanakijiji ambao wanaotumia hospitali ya Ruambwa<br>~ Wanakijiji ambaowanatumia Mradi ya maji ya Dibuoro<br>~ Wanakijiji ambao wanatumia shamba la kijiji | Ardhi | Upatikanaji wa vipande 2,807 vya shamba | Fidia na uhamishwaji |
| 3 | ~ Wanafunzi na wafanyi kazi wa shule mbalimbali<br>~ Wanavijiji wa makanisa mbalimbali,<br>~ Wanavijiji ambao wanaotumia hospitali ya Ruambwa<br>~ Wanakijiji ambaowanatumia Mradi ya maji ya Dibuoro<br>~ Wanakijiji ambao wanatumia shamba la kijiji Kambi wanajeshi | Mijengo | ~ Mijengo 8 za kanisa<br>~ Bloku 1 la darasa<br>~ Vyoo viwili<br>~ Geti mbili pamoja na nyumba 2 za askari<br>~ Ua tatu<br>~ Wire ya faiba ya kambi ya wanajeshi<br>~ Kisima 1 ya kijiji. | ~ Uhamasishaji<br>~ Fidia na Uhamishaji<br>~ Fidia ya mijengo kwa mijengo kwa mashule , ua la hospitali na kisima ya kijiji.<br>~ Eleza kamanda wa wanajeshi kweye kambi. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4 | ~ Watu binafsi,<br>~ Makanisa,<br>~ Mashule,<br>~ Shirika za kijamii<br>~ Serikali za Kaunti. | ~ Kupoteza mapato kutoka kwa biashara<br>~ Biashara hamsini na sita (56) kuathirika | ~ Upotezaji miti elfu arubaini na nne mia nne thelathini na moja (44,431) | ~ Fidia<br>~ Kuunga mkono upandaji miti upya<br>~ Uhamasishaji na utiaji moyo kupanda upya miti iliyopotea |
| 5 | Watu binafsi wanaofanya biashara | Maduka,Uchimbaji wa mchanga mashine ya kusiaga mahindi,vibanda vya mboga na mahoteli | ~ Kupoteza mapato kutoka kwa biashara<br>~ Biashara hamsini na sita (56) kuathirika | ~ Uhamasishaji kwa mahali mbadala<br>~ Fidia na Uhamishaji |
| 6 | Wakulima binafsi wa kilimo cha kujikimu Mazao ya kudumu | Mashamba ya kujikimu yaliyo na mazao | ~ Kaya sabini na moja (71) Kupoteza mazao.<br>~ Kusumbluwa kwa kilimo cha kujikimu na ufugaji | ~ Fidia na Uhamishaji<br>~ Elimu kuhusu mbinu nzuri za kilimo<br>~ Uhamasishaji kuhusu malisho ya hapo hapo na ufugaji wenye tija |
| 7 | Watu binafsi kweye kaya | Makaburi | Makaburi mia tano arubaini na sita (546) | Fidia na uhamishaji wa makaburi |
| 8 | Makundi yenye mazingira magumu (wajane, wenye matatizo ya akili, wazee, wagonjwa, walio kitandani na mayatima. | Ardhi, mijengo, miti, mazao na hali za maisha | ~ Jumla ya kaya elfu moja mia mbili themanini na tatu (1,283) za mazingira magumu zimeathirika.<br>~ Watu elfu tatu mia nne hamsini na moja (3,451) | ~ Urejeshaji wa hali za maisha<br>~ Kugundua Makundi yenye mazingira magumu<br>~ Kunakili changamoto zao |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | walio na mazingira magumu wameathirika.<br>~ Changamoto za kuzoea eneo mpya za kuishi. | ~ Kupeana usaidizi zaidi wakati wa kufidiwa na<br>~ Uhamasishaji<br>~ Kupeana kwa nafasi za kazi |

## 1.14 Vigezo vya kustahiki fidia

Sambamba na Sera za Oparesheni 4.12, watu waliohamishwa wanaweza kugawanywa katika moja ya vikundi vitatu:

- Wale ambao wana haki rasmi za ardhi (ikiwa ni pamoja na haki za kitamaduni zinatambuliwa chini ya sheria za nchi)
- Mdai juu ya ardhi hiyo au mali bora tu madai hayo yanatambulika chini ya sheria za nchi au zinatambuliwa kupitia mchakato ulioelezwa katika mpango wa uhamishaji.
- Wale ambao wana haki ya kisheria ya ardhi wanayoishi.

Wengi wao asilimia themanini na tano nukta mbili (85.2%) ya WMMs wako chini ya kitengo (b) na (c) huku asilimia kumi na nne nukta nane (14.8 %) ya WMMs ikiwa chini ya kitengo (a)

## 1.15 Thamani, Fidia na Haki

### 1.15.1 Kuweka thamani ya mali

Mali zilizoathirika na mradi pendekezi zimeorodheshwa kama ardhi, mijengo, miti, mazao na mali maalum ambazo zimetiwa thamani kulingana na thamani ya sasa ya soko kwa ajili ya fidia:

- Thamani ya ardhi imefikiwa kwa kutumia gharama kamili za ardhi mbadala;
- Thamani ya mijengo imefikiwa kwa kutumia gharama kamili za mali mbadala;
- Thamani ya miti imeongozwa na Shirika la Misitu Kenya (SMK) na thamani katika soko la ndani hivi sasa;
- Thamani ya mazao imeongozwa na ratiba zilizoandaliwa Idara ya Serikali ya Kilimo kwa miaka tofauti na kuzingatia kiwango cha usimamizi.
- Thamani ya upoteza mapato ya kawaida-kama njia ya kurejesha mapato, fidia italipwa kwa wafanyabiashara walioathirika na mradi kiwango cha jumla sawa na mapato ya miezi 6.
- Mali maalum-haswa makaburi kwa shilingi laki moja unusu kwa kila moja. Angalia Kifungu 15.3.3 kwa maelezo kuhusu kima hicho.

Msaada maalum kwa kaya zilizo kwenye mazingira magumu ni Shillingi elfu mia moja.100, 000 kwa kila kaya.

### 1.15.2 Ustahiki

Utafiti wa sensa ulitoa data ambayo inawezesha timu ya utafiti wa WWM kubaini watu walioathirika na mradi (WWMs), Ardhi, rasilimali na biashara, maisha ambayo yataathirika na mradi. Thamani ya ardhi na mali zilizoathirika zimetambulika. Hizi pia zimeorodheshwa katika Jedwali la Ustahiki hapo chini.

**Jedwali 1-5 Ustahiki**

| No. | Aina ya Hasara | Aina ya mali/Matumizi | Mtu stahiki | Aina ya Athari | Fidia ya urejeshali hali |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ardhi | Ardhi ya kilimo | Mmiliki wa ardhi mwenye hati miliki ya kweli au barua za mgao kupitia upatikakana wa kitamaduni au kisheria | Kipande cha ardhi kilichosalia hakina faida kiuchumi | Kipengee cha fidia ya pesa taslimu kwa maeneo ya ardhi yaliyoathirikal<br>Gharama za urejeshaji<br>Uhamasishaji/Uelimishaji wa WWM kuhsu njia mbadala za kilimo zinazoweza kufanywa katika sehemu ya ardhi iliyosalia.<br>Posho ya usumbufu sawa na asilimia kumi na tano (15%) ya thamani ya ardhi |
| | | | Mmiliki wa ardhi mwenye hati miliki ya kweli au barua za mgawo kupitia mgawo wa kitamaduni au kisheria. | Sehemu cha ardhi kilichosalia hakina faida kiuchumi | Ambapo sehemu ya ardhi iliyoathirika ni kubwa na kufanya sehemu iliyobaki kutokuwa na faida kiuchumi eneo lote litanunuliwa na kulipwa fidia za gharama kamili na fidia ya ardhi kwa ardhi itateemea ukubwa Kipande kipya cha ardhi chenye ukubwa sawa na cha awali.<br>Posho ya usumbufu ni asilimia kumi na tano (15%) ya thamani kamili ya ardhi |
| | | Ardhi ya nyumba za kuishi | Wamiliki wa ardhi wenye hati miliki au barua za mgao kupitia magawo wa kitamaduni au kisheria | Ardhi iliyotumika kwa nyumba za kuishi. | Fidia ya pesa taslimu kwa gharama kamili za urejeshaji<br>Posho ya usumbufu ni asilimia kumi na tano (15%) ya thamani kamili ya ardhi |
| | | | Wamiliki wa ardhi wenye hati miliki au barua za mgawo kupitiamgawo wa kitamaduni au kisheria | Ardhi iliyotumika kwa makazi iliyo iliyoharibika yote<br>Sehemu iliyobaki haitoshi kwa matumizi | Iwapo mradi unaathiri nyumba na kipande cha ardhi kinachosalia ni kidogo, ardhi yote inanunuliwa na nyumba hiyo kuhamishiwa katika kipande kingine cha ardhi<br>Hata hivyo iwapo ardhi ni kubwa na nyumba imehamishwa ndani ya ardhi hiyo, fidia ya uhamishaji italipwa kwa gharama kamili za urejeshaji<br>Uhamasishaji wa wenye nyumba zilizoathirika kuhusu uhamishaji na ajira |

| No. | Aina ya Hasara | Aina ya mali/Matumizi | Mtu stahiki | Aina ya Athari | Fidia ya urejeshali hali |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Posho ya usumbufu ni aslimia kumi na tano (15%) ya thamani ya ardhi. |
| | | Ardhi iliyokodiwa | Mpangaji anayetambuliwa na mmiliki wa ardhi kitamaduni. | Upotezaji wa mali katika ardhi ya kukodesha | Fidia ya mali zilipotea kwa bei ya soko<br>Gharama za uchukuzi hadi eneo jipya ya uhamisho.<br>Uhamasishaji/Elimu kwa WWM kuhusu mbinu mbadala za ufugaji |
| | | Ardhi ya malisho | Mmiliki wa ardhi aliye na hati miliki ya kweli | Upotezaji wa ardhi ya malisho na hatimaye kuathiri hali za maisha | Uhamasishaji/Elimu kwa WWM kuhusu mbinu mbadala za ufugaji. |
| | | Shamba la Kukodishwa | Mpangaji anayetambuliwa na mmiliki wa ardhi kitamaduni | Upotezaji wa mali katika ardhi ya kukodi | Fidia ya mali zilizopotea kwa bei ya soko<br>Gharama za uchukuzi hadi eneo jipya ya uhamisho. |
| 2. | Mijengo | Nyumba za kuishi,nyumba za biashara n.k | WWM wanaomiliki aina yoyote ya mijengo katika eneo la mradi ikiwa wana hati miliki ya ardhi au la | Upotezaji wa sehemu au mjengo mzima haswa nyumba za kuishi<br>Uhangaishaji wa watu wanaoishi ndani ya nyumba kupoteza makazi kupoteza biashara | ~ Fidia ya pesa taslimu kwa kila mwenye mjengo ikiwa wanamiliki shamba au la<br>~ Fidia ya mijengo itakuwa kwa bei ya soko.<br>~ Uhamasishaji/Elimu kwa WWM kuhusu mbinu mbadala<br>~ Nafasi ya kuokoa vifaa<br>~ Nafasi ya kila muathiriwa kuchukua mabakio za nyumba yake ama jingo lake.<br>~ Notisi ya miezi 3 ya kuhama.<br>~ Posho ya usumbufu ni aslimia kumi na tano (15%) ya thamani ya ardhi. |
| 4 | Kupoteza kwa riziki kutoka kwa biashara | Riziki kutoka kwa nyumba za kukodesha | WWM ambao wako na mijengo ambazo zinatumika kama duka, mijengo za kuishi, hoteli. WWM ambao wako na viti na | Kupoteza riziki kwa mda wa miezi 6 | ~ Fidia ya pesa taslimu<br>~ Fidia ya pesa taslimu ya mapato ya kila mwezi kwa muda wa miezi sita (6)<br>~Usaidizi wa kutafuta eneo mbadala ya kuanzisha tena Biashara |

| No. | Aina ya Hasara | Aina ya mali/Matumizi | Mtu stahiki | Aina ya Athari | Fidia ya urejeshali hali |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | mahema za kukodesha. | | ~ Uhamasisho na mafundisho wa WWMs kwa njia mbada za biashara<br>~ Posho ya usumbufu ya asilimia kumi na tano (15%) ya mapato ya kila mwezi<br>~ Notisi ya mwezi (tatu) 3 ya kuwezesha kuhamia eneo mbadala na kuanzisha Biashara zao tena |
| | | Riziki kutoka kwa maduka madomadogo | Wauzaji wa bidhaa mbalimbali | Kupoteza kwa riziki kwa muda wa miezi 6 | ~ Fidia ya pesa taslimu<br>~ Fidia ya pesa taslimu ya mapato ya kila mwezi kwa muda wa miezi sita (6)<br>~ Usaidizi wa kutafuta eneo mbadala ya kuanzisha tena Biashara<br>~ Uhamasisho na mafundisho wa WWM kwa njia mbadala za biashara<br>~ Posho ya usumbufu ya asilimia 15% ya mapato ya kila mwezi<br>~ Notisi ya mwezi tatu (3) ya kuwezesha kuhamia eneo mbadala na kuanzisha Biashara zao tena |
| | | Riziki kutoka kwa maduka za huduma ka ma vile kinyozi,duka za kungenezea baiskeli n.k | Waliopeana huduma | | ~ Fidia ya pesa taslimu<br>~ Fidia ya pesa taslimu ya mapato ya kila mwezi kwa muda wa miezi sita (6)<br>~ Usaidizi wa kutafuta eneo mbadala ya kuanzisha tena Biashara<br>~ Uhamasisho na mafundisho wa WWMs kwa njia mbada za biashara<br>~ Posho ya usumbufu ya asilimia kumi na tano (15%) ya mapato ya kila mwezi<br>~ Notisi ya mwezi tatu (3) ya kuwezesha kuhamia eneo mbadala na kuanzisha Biashara zao tena |
| | | Wauzaji mchanga | Waliouza mchanga katika eneo la mradi | Kupoteza riziki kutokakana na uuzaji wa mchanga kutoka kwa mto Nzoia | Njia ama sehemu za mpito yameachiliwa kwa wafanyi Biashara hawa |

| No. | Aina ya Hasara | Aina ya mali/Matumizi | Mtu stahiki | Aina ya Athari | Fidia ya urejeshali hali |
|---|---|---|---|---|---|
| 5. | Miti | Mbao, vifaa vya Ujenzi, dari linalotoa kivuli<br>Miti ya matunda | Wamiliki wa miti iwapo wanamiliki ardhi au laa | Upotezaji wa mbao kwa ajili ya fanicha<br>Upotezaji kivuli ndani ya ua la WWM<br>Upotezaji wa vifaa vya ujenzi<br>Upotezaji wa chakula na mapato kutokana na mauzo ya matunda | ~ Fidia ya miti iliyoathirika na mradi inaongozwa na viwango vya serikali la Miiti Kenya<br>~ Uhamasisho na mafundisho wa WWMs kuhusu uzuru wa upanzi tena wa miti<br>~ Posho ya usumbufu ya asilimia kumi na tano (15%) ya bei ya mti |
| 6. | Mazao ya kudumu | Chakula cha kujikimu kwa wakulima<br>Chanzo cha mapato kinapopelekwa sokoni | Mmiliki wa mazao iwapo anamili ardhi au la | Upotezaji wa mazao ya chakula kwa mkulima<br>Upotezaji mapato | Fidia ya mazo ya kilimo kama inavyoongozwa na viwango vya Wizara ya kilimo na thamai ya mazao hayo katika soko.<br>Uhamashishaji na elimu kwa WWM kuhusu urejeshaji kupitia kupanda miti |
| | Upotezaji mapato | Athari kwa makundi yenye mazingira magumu | Kaya zote zenye watu walioko na mazingira magumu | | Watu wote wenye mazingira magumu wanahitaji msaada wa urejeshaji hali za maisha kama ilivyoainishwa katika kifungu 12 |
| 7. | Ardhi ya Jamii<br>Shamba la Serikali<br>Shamba, Miti, Choo za Shimo, Nyumba, Vizuizi ya Shule, Nyumba na Geti la kituo cha afya<br>Shamba, Jumba, Miti na Choo la shimo la Kanisa<br>Mradi wa Kijamii (Kisima) | Shamba la Umma<br>Taasisi za Kujifunza<br>Vituo vya Afya vya kuhudumia jamii<br><br>Kisima cha maji cha jamii | Jamii walioathirika na mradi<br>Idara za Serikali zinazotumia shamba<br>Waekezaji wa Mashule<br>Vituo vya Afya vinavyo simamiwa na Serikali ya KauntiWanachama wa vikundi vya msaada | Upotezaji mapato | Malipo ya pesa kwa wanao athiriwa Mashamba na nyumba zao kwa gharama kamili ya uingizwaji<br>Sehemu ya Kanali inayopitia katika shule and kituo cha afya ambazo ni taasisi za umma.<br><br>Kanali zilizofungwa zimependekezwa katika sehemu hizi. Ujenzi wa Shule kwa Ujenzi wa Shule kwa shule zilizo athirika na mradi<br>Ujenzi wa haraka wa bomba la kusambaza maji masafi ya jamii na wodi ya kituo cha afya |

| No. | Aina ya Hasara | Aina ya mali/Matumizi | Mtu stahiki | Aina ya Athari | Fidia ya urejeshali hali |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kitalu cha miti and kizuizi cha kikundi cha msaada | | | | |
| | Maeneo matakatifu/ya kitamaduni | Makaburi | Ndugu/jamaa wa aliyefariki | Mshikamano thabiti kati ya walio hai na waliofariki<br>Hofu ya kuwasumbua waliofariki wasije kuleta mikosi | Fidia ya kuhamisha makaburi itahusisha yafuatayo:<br>Mpango wa sherehe na wanafamilia na viongozi wa kitamaduni<br>kufanya matambiko ya kitamaduni kwa ajili ya uzikaji upya<br>Cheti kutoka kwa serikali kuchimba maiti<br>Pesa kima cha shilingi elfu mia moja hamsini (Ksh.150,000) kama gharmna fidia ya kuhamisha makaburi |

## 1.16 Kupunguza gharama ya uhamishaji

Muundo wa kina wa Lahmeyer International / GFA Consultants na Quadrant Consulting Engineers wa Juni 2017 umetengenezwa kuinyoosha mifereji ili kuzuia au kupunguza usumbufu wa uhamishwaji unaotokana na mradi huo kwa kufuata sera ya uendeshaji ya Benki ya Dunia Sera za Operesheni 4.12. Hatua zingine ambazo zimechukuliwa ili kupunguza athari za mradi ni pamoja na:

Muundo wa mwisho uajumuisha madaraja, njia za miguu, ngazi na sehemu ya maji kuhakikisha ufikiaji wa mara kwa mara baina ya jamii ,na ufikiaji wa mto kwa mahitaji yote ya nyumbani,mifugo,wavunaji mchanga na shughuli za uvuvi.

Barabara zimejumuishwa pembezoni mwa mifereji (Mifereji mikuu) ili kupunguza usumbufu wa kijamii na uharibifu wa mazingira.

Wale wote watakaoathirika na mradi watafidiwa kikamilifu kabla ya mradi kuanza.

WWM ambao watahitajika kuhamishwa watapewa notisi ya mapema (miezi 3) kuhakikisha wanajenga nyumba mpya na kurahisisha uhamaji mzuri na walio kwenye mazingira magumu watapewa chaguzi ya kujijengea nyumba mpya wenyewe au wajengewe itategemea watakavyotaka.

## 1.17 Mfumo wa kitaasisi wa utekelezaji wa MUU

Mijengo ya mradi wa umwagiliaji wa Lower Nzoia- 1 na ile ya Kinga Dhidi ya Mafuriko ya Nzoia inatekelezwa na Mradi wa Kenya wa Uhakika wa Maji Ujasiri wa hali ya Anga (KWSCRP) kwa kushirikiana na Bodi ya Kitaifa Umwagiliaji (BYU) kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji (MOWI).

Wizara ya Maji na Umwagiliaji itaongeza fedha kutoka kwa serikali ya Kenya kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Uhamishwaji (MUU) (Fidia na uhamishaji wa WWM). Jukumu la jumla la fidia inachukuliwa na mdhamini wa mradi, Serikali ya Kenya kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Kitengo cha kusimamia mradi, Bodi ya Kitaifa Umwagiliaji watasimamia utekelezwaji wake. Utekelezaji wa malipo ya fidia kwa WWMs wakati wa uhamsihwaji kama mojawapo ya majukumu yao makuu

### 1.17.1 Kamati za uhamishaji na Fidia za Kaunti ndogo (KUFKNs)

Kamati za uhamishaji na fidia za kaunti ndogo (KUFKNs) hazitahusika katika upatikanaji wa ardhi au fidia kwa sababu hili linasalia kuwa jukumu la.Kila moja ya kaunti ndogo 2 zilizoathirika na MULN zitaunda kamati ya KUFKN. PMU itasaidia kuunda KUFKN pamoja na ofisi za ardhi katika ngazi za kaunti ndogo ambayo itaongozwa na Naibu Kamishna wa Kaunti (NKK). KUFKN itaisaidia Kamisheni ya Kitaifa ya Ardhi (KKA) / Kitengo cha kusimamia mradi (KKM)/ Bodi ya Kitaifa Umwagiliaji (BYU) kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi; haswa kuhakikisha mawasiliano ya kufana kati ya KKA na jamii zilizoathirika. Wanachama wa Kamati za uhamishaji na fidia za kaunti ndogo (KUFKN) watajumuisha uwakilishi kutoka mashirika yafuatayo:

- Mwakilishi wa Utawala wa Kaunti ndogo, ambaye hapa atakuwa Naibu Kamishna wa Kaunti na atatoa uhamasishaji wa jamii unaohitajika sana, na kuunga mkono mradi katika mchakato wa

uhamishaji. Naibu Kamishna wa Kaunti ataongoza kamati za KUFKNs katika kila kaunti ndogo; mwakilishi wa Kitengo cha kusimamia mradi

- kama shirika linalotekeleza mradi wa unyunyizaji wa Lower Nzoia;
- Afisa wa uchunguzi wa ardhi wa kaunti ndogo atakayesaidia katika shughuli za usoroveya na mipaka ya ardhi itakayopatikana;
- Mwakilishi wa Serikali ya Kaunti katika ngazi ya kaunti ndogo;
- Mwakilishi wa WWMs aliyetambulishwa na kamati ya kata ya uhamishaji na fidia-awe kama sauti ya walioathirika na mradi WWM. Kila moja ya kata 2 itachagua wawakilishi (mume na mke) kuwa sehemu ya kamati nne za Kamati za uhamishaji na fidia za kaunti ndogo
- Mashirika Yasiyo ya Serikali na Asisi za Kijamii zinazoshiriki kikamilifu kuhakikisha WWM wanasaidiwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa Uhamishwaji MUU na kusaidia katika kurejesha hali za maisha, utoaji habari, miongoni mwa mambo mengine.

WWM watachagua mwakilishi wao kwa KUFKN ilhali Afisa wa Jamii na Jinsia wa kaunti ndogo watachagua Mashirika Yasiyo ya Serikali au Asisi za Kijamii changamfu katika eneo hilo. KUFKN itakuwa na majukumu maalum yafuatayo kuhusu utekelezaji wa MUU:

- Kuhakikisha mtiririko wa habari unaofaa kati ya Tume ya kitaifa ya ardhi, Kitengo cha kusimamia mradi na WWMs
- Kuratibu kamati za kata za uhamishaji na fidia (KKUFs);
- Kuthibitisha hesabu za WWMs na mali zilizoathirika;
- Kuongoza na kufuatilia utekelezaji wa uhamishaji
- Kuratibu shughul kati ya mashirika mbalimbali yanayohusika na uhamishaji
- Kuwezesha utatuzi wa malalamiko na migogoro
- Kusaidia na shughuli za kurejesha hali za maisha

### 1.17.2 Kamati za Kata za Uhamishaji na Fidia (KKUFs)

Kamati za kata za uhamishaji na fidia (KKUFs), zilizoko katika kila kata zimeundwa na kukubaliwa. KKUFs ziliundwa na timu ya Mshauri kwa msaada wa utawala wa mitaa kutoka tarehe 21- 22 Julai mwaka wa elfu mbili kumi na saba (2017) ndani ya eneo la MUU III.  Kuratibu kamati za kata za uhamishaji na fidia (KKUFs) zitafanya kazi chini ya uongozi na uratibu wa KKUF. Uanachama wao unajumuisha wafuatao:

Chifu, ambaye ni mwakilishi wa serikali katika ngazi ya kata na ambaye anahusika na migogoro ya kijamii ataiwakilisha serikali katika kamati ya

- Naibu Chifu, ambaye anamsaidia Chifu wa kata na serikali katika kusimamia migogoro ya jamii katika vijiji, atakuwa mwanachama pia.
- Mtu aliye athirika na mradi mwanamke, atakayechaguliwa na WWMs wanawake, atawakilisha masuala ya wanawake na watoto kuhusu uhamishwaji na fidia
- Mwakilishi wa vijana, atakayechaguliwa na vijana, atawakilisha masuala ya vijana katika Kuratibu kamati za kata za uhamishaji na fidia
- Mwakilishi wa watu walio na mazingira magumu, atashughulika na kuwakilisha masuala ya watu wenye mazingira magumu katika Kuratibu kamati za kata za uhamishaji na fidia.
- Mwakilishi wa wafanyi biashara, atawakilisha masuala ya wanabiashara.
- Mwakilishi wa Chama cha Watumizi wa Maji ya Umwagiliaji (CWMU), ikiwa kipo katika kata hiyo.

Wanachama katika KKUFs walichaguliwa kwa kila kitengo cha WWMs isipokuwa Chifu wa kata na manaibu wa chifu ambao ni wanachama wa moja kwa moja wa timu hiyo kutokana na kazi zao. Kila Kuratibu kamati za kata za uhamishaji na fidia ilichagua mwenyekiti na Katibu. Majukumu ya Kuratibu kamati za kata za uhamishaji na fidia yatajumuisha miongoni mwa mambo mengine yafuatayo:

- Kufanya uhamasishaji mkubwa wa umma na mashauriano na watu walioathirika.
- Kusaidia kuhakikisha kuwa malalamiko yaliyotolewa na WWM kuhusu uhamishwaji na fidia miongoni mwa mengine yanashughulikiwa ipasavyo na mamlaka husika
- Kusaidia kufanya kazi kwa ufanisi kwa washauri wa Uhamishwaji MUU katika uthibitishaji na usasishaji wa Uhamishwaji MUU baada ya utafiti wa kina kukamilika.
- Kutatua migogoro ambayo inaweza kutokea inayohusu mchakato wa uhamishwaji na fidia. Ikiwa itashindwa kutatua, itasaidia kupeleka malalamiko hayo kwa KUFKN.
- Kuhakikisha kuwa malalamiko ya watu walio kwenye mazingira magumu kama vile wasiojiweza, wajane, mayatima walioathirika yanashughulikiwa.
- Kusaidia walio kwenye mazingira magumu wakati wa fidia na urejeshaji hali za maisha. Kuhakikisha WWM wote katika eneo lao wanafahamishwa kuhusu yaliyomo kwenye Uhamishwaji MUU.

## 1.18 Kushughulikia malalamiko

Wakati wa mikutano ya wazee (MYW), timu ya utafiti ilihoji kuhusu mapendekezo bora ya fidia ili kukwepa utokeaji wa matatizo wakati wa fidia, kama vile vita vya kifamilia na migogoro. Wanachama walikubaliana kuwa njia bora zaidi ni kupitia utawala wa mitaa iwapo tatizo halikutatuliwa katika ngazi ya familia.

Muundo wa asasi ya utatuzi wa migogoro ambayo ilijadiliwa na waliohudhuria ni kama ifuatavyo.

- Chifu alipewa jukumu la kuwaita wanachama wote walio na migogoro na kutatua matatizo yanayotokana na fidia.
- Chifu atapokea hundi za wanachama wote waliokubali kufidiwa.
- Kwa wale ambao hawajakubalina kuhusu jinsi ya kugawana pesa/wana mizozo mingine, pesa hizo zitawekwa katika akaunti ya pesa zilizoshikiliwa na mtu wa tatu kwa niaba ya wahusika wanaofanya biashara katika kamisheni ya Kitaifa ya Ardhi.
- Kulingana na makubaliano na suluhu iliyofikiwa na familia zenye migogoro, chifu ataiandikia barua benki na kuishauri kuhusu jinsi ya kuzigawa pesa miongoni mwa wanufaika.

Hii inamaanisha kwamba Chifu wa eneo atapewa majukumu makuu ya usimamizi ndani ya utaratibu wa utatuzi wa malalamiko.

Matokeo ya Mazungumzo ya vikundi pia iliibua maoni kwamba wakati utaratibu uliopendekezwa wa malalamiko unapaswa kupitia kwa utawala wa mitaa, wanachama wengine wa utaratibu huo wanafaa kujumuishwa wawakilishi wa watu walioathirika na mradi WWMs kutoka kata zote zilizoathirika pamoja na wataalamu wa ndani na nje.

Utaratibu wa malalamiko ufuataо umependekezwa kwa utekelezaji wa mpango huu wa Uhamishwaji MUU.

### 1.18.1 Ngazi ya kwanza: Kamati ya mtaa

Kamati ya malalamiko ya mtaa imeundwa katika ngazi ya mtaa na inajumuisha wanachama wafuatao:

- Mwenyekiti: Mwakilishi Wadi;
- Katibu: Chifu wa Eneo;
- Msimamizi wa Wadi;
- Mzee wa mtaa ambao WWM wenye malalamiko wanatoka;
- Wanachama: Wawakilishi wanne wa WWM kukiwa na mwanaume, mwanamke na kijana (miaka 18 hadi 30) na mzee.
- Mtu aliyeathirika na mradi WWM kutoka kwa wawakilishi kuwa kama kiunganishi.

Kamati hii itafanya kikao katika ofisi ya mwakilishi wa wadi kila baada ya wiki mbili. Utaratibu ufuatao unapendekezwa:

Mtu aliyeathirika na mradi MMU anaandikisha malalamiko yake na ndani ya siku moja, wanachama wa kamati wanaelezwa kuhusu suala hilo.

1) Mtu aliyaethirika anafahamishwa kuhusu tarehe ijayo ya kusikizwa kwa malalamiko yake. Kulingana na wingi wa kesi, tarehe inafaa kuwa ndani ya siku saba za kazi kati ya tarehe ambayo malalamiko yameandikishwa na siku ya kusikizwa.
2) Kamati inakutana mara moja katika wiki kushughulikia kesi zinazochipuza. Katika vikao hivi, kesi zitasikizwa na mashahidi kuitwa
3) Kamati itatoa uamuzi wake kwa watu walioathirika ndani ya siku tatu za kazi;
4) Ikiwa hakuna azimio lolote lililofikiwa au MMU hajaridhika na uamuzi, kamati itaipeleka kesi hiyo katika ngazi nyingine.Hii itafanyika ndani ya siku tano 5 za kazi baada ya kusikizwa;
5) Ikiwa MMU hajaridhika na uamuzi, ataruhusiwa kupeleka kesi hiyo katika ngazi nyengine.

### 1.18.2 Ngazi ya pili: Kamati ya Kaunti

Malalamiko mengine yanaweza kuhitaji kuitwa kwa mashahidi, kutoelemea upande wowote au tathmini ya kiufundi kabla ya kupendekeza suluhisho. Taratibu za mitaa zinaweza kukosa uwezo wa kufikia mahitaji yote haya na hivyo kutahitajika msaada.

Kamati ya ngazi ya Kaunti iliyo na wanachama wafuatao inapendekezwa:

- Mtu anayeheshimika katika jamii kama vile kiongozi wa dini au kiongozi wa jamii aliyechaguliwa na WWMs;
- Mwakilishi maalum kutoka bodi ya kitaifa ya umwagiliaji / unyunyizaji;
- Mwakilishi maalum kutoka Wizara ya Maji;
- Mwakilishi maalum kutoka Ofisi ya kitengo cha kusimamia mradi
- Mwakilishi kutoka serikali ya kaunti k.m Afisa Mkuu Wizara ya Ardhi;
- Naibu Kamishna wa Kaunti (NKK);
- Wanachama: Wawakilishi watatu wa WWM wakiwemo mwanaume, mwanamke na kijana.
- Mtu aliyeathirika na mradi ambaye amechaguliwa miongoni mwa wawakilishi kuwa kama kiunganishi.

Kamati hii itaongozwa na kiongozi wa dini lakini katibu aliyependekezwa atakuwa ama Kamishna wa kaunti ndogo au mwakilishi wake.
Kamati hii pia inaweza kumualika msomi au wawakilishi waliohitimu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika ngazi ya kaunti wengine kutoka kwenye wizara pia wanaweza kualikwa kutoa ushauri wa kitaalamu kadri hitaji linavyotokea. Hawa wanaweza kuwa maofisa kutoka Wizara ya ardhi nyumba na maendeleo ya miji (MLHUD) kama vile Soroveya wa Wilaya wa Ardhi na/au Msajili wa Ardhi wa Wilaya.

Kamati itafanya kikao katika ofisi ya Serikali ya Kaunti mara moja kwa mwezi au Hitaji litakapotokea.

Utaratibu ufuatao unapendekezwa:

Malalamiko yanatumwa kutoka ngazi ya mitaa na kupokewa ofisi ya serikali ya kaunti.Hii inajumuisha kesi zilizotumwa kutoka ngazi kamati ya mitaa;

1. Ndani ya siku tano za kazi, notisi inatumwa kwa wahusika wote kuwafahamisha kuhusu tarehe ya kusikizwa kwa kesi;
2. Kabla ya kusikizwa kesi, mwenyekiti na katibu wataamua hitaji la mpatanishi na kumualika wakati wa kusikizwa kesi;
3. Kesi itasikizwa ndani ya siku ishirini baada ya lalamiko kutolewa;
4. Katika kesi ambapo mpatanishi anahitajika, uamuzi wa kamati ni wa mwisho. Mlalamikaji anapaswa kufahamishwa hivyo mapema;
5. Uamuzi unafaa kuwasilishwa ndani ya siku tano (5) za kazi;
6. Migogoro isiyoweza kutatulika katika ngazi hii inafaa kupelekwa kwa kamati nyingine ndani ya siku tano.

### 1.18.3 Ngazi ya tatu: Kamati ya mradi

Malalamiko mengine yanaweza kutokea kuwa yako nje ya udhibiti wa moja kwa moja wa Kamati ya Utekelezaji wa Mpango wa uhamishwaji KMUU na yatahitaji kushughulikiwa katika ngazi za sera za kitaifa au kaunti. Hii inajumuisha malalamiko ambayo yanahitaji ufafanuzi au uchunguzi kabla ya kufikia suluhisho. Katika kesi kama hizo, KMUU huenda itahitaji ufafanuzi wa kisheria kuhusu baadhi ya mambo.

- Kamati ya Ngazi ya Mradi inayoundwa na wanachama wafuatao inapendekezwa:
- Mwenyekiti: Afisa Mtendaji Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Mji;
- Katibu: Kamishna wa Kaunti;
- Mwakilishi maalum kutoka kitengo cha kusimamia mradi
- Mwakilishi maalum kutoka Tume ya Kitaifa ya Ardhi;
- Wanachama: wawakilishi watatu wa MMU wakijumuisha mwanaume, mwanamke na kijana.

Kamati hii itafanya kikao katika Ofisi za serikali ya Kaunti mara moja kila baada ya miezi mitatu. Utaratibu ufuatao unapendekezwa:

1. Malalamiko yanaandikishwa katika Ofisi za serikali ya kaunti na ndani ya siku tano za kazi. Notisi inatolewa kwa wahusika wote kuwataarifu kuhusu tarehe ya kusikizwa kwa kesi.Hii inajumuisha kesi zilizoletwa kutoka ngazi ya kamati ya kaunti;
2. Kesi itasikizwa ndani ya siku thelathini ya kuandikishwa kwa malalamiko;
3. Ikiwa uchunguzi na mashahidi wa kiufundi wanahitajika, itachukua sio zaidi ya siku thelathini kabla ya kesi kusikizwa;
4. Uamuzi wa kamati utawasilishwa kupitia maandishi ndani ya siku 5 ya tarehe ya kusikizwa;
5. Ikiwa kamati haitatatua suala, watu walioathirika wako huru kwenda katika mahakama ya Ardhi na Mazingira.

Kwa kuzingatia ngazi tofauti za kutoa uamuzi zinazohitajika katika hatua hii, inapendekezwa kuwa uamuzi wa mwisho kutoka kwa kamati hii uwasilishwe ndani ya miezi mitatu (robo ya mwaka wa kifedha).

## 1.19 Uhamishwaji wa kaya zilizotengwa kabisa KZ

MMU 11 ambazo kaya zake zimeathirika na mradi (ambapo kati yazo kuna kaya mbili (2) za walio na mazingira magumu) na watahitajika kuhamishwa kabisa wameonyesha yafuatayo:

- Wako tayari kuondoka sehemu hiyo kwa sababu mradi utazalisha kipato kwa jamii na kuimarisha uhakika wa chakula;
- Upendeleo wa kwanza wa kuhama ni ndani ya jamii yao ambapo wamejenga uhusiano mwema na kila mmoja anamuelewa mwenzake na wako tayari kusaidiana shida inapotokea. Kuhamishwa katika eneo tofauti kutaleta changamoto kwa wazee.

Wakati wa mikutano kadhaa ya mashauriano ilielezwa kuwa ardhi inapatikana katika makubaliano ya mnunuaji na muuzaji. Katika eneo la mradi kuna fursa za kununua ardhi kutoka kwa wale walio na zaidi ya kipande kimoja cha ardhi.
MMU pia walisema watapenda kulipwa pesa halafu wajitafutie ardhi wenyewe.
Muhtasari wa kaya zilizoathiriwa na kupoteza makao unaonyeshwa katika jedwali hapo chini.

**Jedwali 1-6: KZ waliopoteza makao kabisa**

| Bloku/Sehemu | Idadi ya KZ waliopoteza makazi | Idadi ya KZ wenye mazingira magumu waliopoteza makao |
|---|---|---|
| B1 | 8 | 1 |
| B2 | 0 | 0 |
| B3 | 1 | 1 |
| B4 | 6 | 3 |
| B5 | 8 | 2 |
| B6 | 2 | 0 |
| B7 | 24 | 11 |
| SC6 | 5 | 2 |
| SC8 | 8 | 6 |
| SC9 | 0 | 0 |
| SC11 | 1 | 0 |
| SC12 | 15 | 9 |
| SC13 | 9 | 4 |
| SC14 | 16 | 14 |
| MD1 | 2 | 1 |
| MD2 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **105** | **54** |

Ijapokuwa wenye kaya zilizoathiriwa wanapendelea zaidi fidia ya pesa taslimu, hii inaweka ustahiki wa kaya nzima katika hatari ya kutumiwa vibaya na pia kuna hatari ya kuchelewesha mradi kwa sababu wanahitajika kuondoka katika sehemu la upokeaji ujenzi kuanza.

Kwa sababu hiyo, wenye kaya zilizoathiriawa mia moja na tano (105) watasaidiwa na kuwezeshwa na mradi kupata ardhi mpya na kulipiwa, halafu kitakachosalia watapewa pesa taslimu kama wanavyotaka.

Kaya (mbili) 2 walio kwenye mazingira magumu zitapata msaada wa ziada/msaada kama ilivyoainishwa katika Vifungu 6.3.10 na 12.2.9.

## 1.20 MMU III Makadirio ya jumla ya gharama

Thamani ya mali zilizoathirika ndani ya utafiti wa eneo la MMU III lenye ukubwa wa ekari mia moja tisini na sita (**196)** ni Shillingi Milioni elfu mia tisa arubaini na nane, Mia mbili arubaini na moja, Mia mbili na kumi na nane **KShs. 948,241,218.00 (**ikijumuisha asilimia kumi na tano (15%) na asilimia kumi (10%) gharama za utekelezaji na dharura mtawalia) Usambazaji wa thamani ya fidia umewasilishwa katika jedwali 1-8 hapa chini.

**Table 1-7: Muhtasari wa Mali zilizoathirika na gharama – Sehemu ya unyunyizaji**

| **No.** | **Mali** | **Idadi ya wenye mali** | **Ukubwa wa mali iliyoathirika (Ekari)** | **Idadi zilizoathirika** | **Jumla (KShs.)** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Shamba | 2,807 | 485 | 2,807 | 139,483,999.00 |
| 2 | Mijengo | 697 | - | 1,382 | 350,948,460.00 |
| 4 | Bishara | 49 | - | 56 | 7,489,000.00 |
| 5 | Miti | 967 | - | 44,431 | 71,209,016.00 |
| 6 | Mimea | 71 | - | Mazao mbalimbali | 793,700.00 |
| 7 | Makaburi | 181 | - | 546 | 81,900,000.00 |
| | **Jumla ndogo 1 (KShs.)** | | | | **651,824,175.00** |
| 8 | Posho ya kisheria ni asilimia kumi na tano (15% of Sub-total) | | | | 97,773,626.00 |
| | **Jumla ndogo 2 (KShs.)** | | | | **749,597,801.00** |
| 9 | Gharama za utekelezaji ni asilimia kumi na tano (15%) | | | | 112,439,670.00 |
| | **Jumla ndogo 3( Kshs)** | | | | **862,037,471.00** |
| 10 | Ongeza asilimia kumi (10%) gharama | | | | 86,203,747.00 |
| | **Hesabu ya Jumla** | | | | **948,241,218.00** |

Kutokana na mchakato wa pole pole wa uamuzi wa ardhi, usasishaji wa sajili za ardhi na kukosekana kujitolea kwa wenye ardhi kubadilisha rekodi za ardhi, nusu ya vipande vya ardhi vilivyoathirika vimesajiliwa chini ya wamiliki wa awali ambao baadhi yao washafariki. Baadhi ya vipande vya ardhi vinamilikiwa kama bloku (ugawaji wa ardhi umefanyikamashinani tu lakini rekodi hazijabadilishwa).

## 1.21 Urejeshaji wa hali ya Maisha

### 1.21.1 Kanuni muhimu zinazoongoza mpango wa marejesho ya hali za maisha

Njia endelevu za urejesho wa hali za maisha unafuata kanuni zifuatazo:

- Hali za maisha ni mikakati ya pande nyingi na mchanganyiko wa njia unahitajika ili kusaidia urejeshaji wa mapato na uanzishaji upya wa mitandao ya misaada ya kijamii;
- Ushiriki kikamilifu wa walengwa waliokusudiwa katika kupanga na kufanya maamuzi ili kuhakikisha msaada uliopendekezwa unaonyesha hali halisi ya eneo;
- Wale Walioathirika na Mradi wanapaswa kuchaguwa wenyewe ili waweze kuamua ni jinsi gani kaya zao zitanufaika na chaguzi zilizopo za urejeshaji wa hali za maisha;
- Kaya zilizo katika mazingira ahatarishi haziwezi kuzoea mabadiliko na kwa hivyo zinahitaji msaada unaolengwa kupitia upangaji na utekelezaji wa urejeshaji wa hali za maisha.
- Posho za mpito ni muhimu, lakini zinahitaji ustahiki wa wazi.
- Kukuza uwezo kunapaswa kuingizwa katika shughuli za urejeshaji wa hali za maisha ili kukuza ujuzi wa Wale Walioathirika na Mradi, pamoja na usimamizi wa fedha. Uongezaji uwezo unatambua mahitaji tofauti ya wanawake, wanaume, vijana na makundi ya walio kwenye mazingira magumu.

### 1.21.2 Mpango uliopendekezwa wa urejeshaji hali za maisha

Mpango wa urejeshaji hali za maisha, MUHM, umeunganishwa na rasilimali zilizopo, maarifa, ujuzi na uzoefu wa kaya. Mipango tofauti ya urejeshaji wa hali za maisha inapendekezwa kutekelezwa na mteja kwa msaada wa mashirika husika ya serikali na uongozi wa jamii.MUHM ina vipengee anuwai:

- Fidia na uhamishwaji;
- Utoaji waharaka wa msaada wa mpito;
- Uwezo wa kukuza kilimo/ msaada wa hali za maisha unaotegemea ardhi;
- Msaada wa mtaji na uendelezaji wa biashara ndogo;
- Mafunzo ya usimamizi wa fedha;
- Utoaji wa ajira kwa wenyeji wakati wa awamu ya ujenzi;
- Utoaji mafunzo na msaada kuhusu uhamasishaji wa VVU/Ukimwi

Mipango wa urejeshaji hali za maisha zilizopendekezwa zinafafanuliwa katika kifungu 12.

### 1.21.3 Mpango wa urejeshaji hali za maisha (MUHM) makadirio ya gharama

Makadirio ya gharama za Mipango wa urejeshaji hali za maisha kwa ajili ya MUU III ni **Millioni mia tatu nukta sita (Kshs 300.6 million)** kama ilivyoainishwa katika jedwali hapo chini

**Jedwali 1-8 : Makadirio ya msaada wa urejeshaji hali za maisha**

| Shughuli/Maelezo | Muda | Makadirio ya Bajeti(KES) | Maoni |
|---|---|---|---|
| Ujenzi wa nyumba (takriban nyumba 54 za watu wenye mazingira magumu @ 2.5 million) | 6 miezi | 135,000,000.00 | Fidia na serikali ya Kenya |
| Msaada wa mpito kwa kaya 1,283 wenye mazingira magumu @ 100,000 | - | 128,300,000.00 | Benki ya Dunia |
| Msaada wa uwezo wa kilimo | Miaka 7 | 0.00 | KfW |
| Usimamizi wa fedha-Kwa wote | Miezi 3-6 | 5,000,000.00 | Inafhadhiliwa na Benki ya Dunia /KfW na kusimamiwa na kitengo cha kitengo cha kusimamia mradi |
| Washauri wa nje | Baada ya kila miezi 6 | 5,000,000.00 | Inafhadhiliwa na Benki ya Dunia /KfW na kusimamiwa na kitengo cha kitengo cha kusimamia mradi |
| **Jumla ndogo** | | **273,300,000.00** | |
| Ongeza 10% gharama | | 27,330,000.00 | |
| **Hesabu Jumla** | | **300,630,000.00** | |

## 1.22 Muhtasari wa matokeo ya utafiti wa MUU

**Jedwali 1-11 Maelezo ya jumla yanayotoa mukhtasari wa matokeo ya utafiti wa MUU**

| No | Vitu | | | Nambari |
|---|---|---|---|---|
| A | **Idadi ya walioathiriawa** | | | |
| | Idadi ya jumla ya wenye mali walioathiriwa (Watu binafsi, kaya na taasisi) | | | 3,229 |
| | Idadi ya WWM | **Jumla** | | **12,561** |
| | | Watu wazima | Wanaume | 3,816 |
| | | | Wanawake | 2,806 |
| | | Watoto | Wanaume | 1,790 |

| No | Vitu | Nambari | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | 1,600 |
| | | Hawajaainishwa (watu wazima au watoto) | Wanaume | 959 |
| | | | Wanawake | 419 |
| | | Jinsia (haibainishwa)) | | 1,171 |
| | Kundi la watu wenye mazingira magumu | **Kaya zilizoathirika** | | **1,283** |
| | | Wazee | | 655 |
| | | Wenye matatizo ya akili | | 187 |
| | | Mayatima | | 418 |
| | | Wasiojiweza | | 428 |
| | | Wagonjwa mahututi au wagonjwa (pumu, kifafa, Anemia selimundu,n.k) | | 567 |
| | | Wagonjwa ( Ukimwi ) | | 677 |
| | | Wajane | | 519 |
| | WWM waliokosa makazi kabisa | | | 105 |
| **B** | **Ardhi iliyoathirika** | | | |
| | Idadi kamili ya vipande vya ardhi vilivyoathirika | | | 2,807 |
| | Vipande vya ardhi vinavyomilikiwa na watu binafsi | | | 2,788 |
| | Shule/chuo | | | 7 |
| | Serikali za Kaunti | | | 3 |
| | Makanisa | | | 8 |
| | Ardhi ya jamii | | | 1 |
| | Jumlaa ya ukubwa wa ardhi iliyochukuliwa sehemu ya MUU III | | | 196 ha/ 486 ekari |
| | Thamani ya jumla ya ardhi iliyoathirika | | | Kshs 139,483,999.00 |
| **C** | **Mijengo iliyoathirika** | | | |
| | Idadi kamili ya kaya zenye mijengo zilizoathirika | | | 697 |
| | Idadi kamili ya mijengo iliyoathirika | | | 1,382 |
| | Thamani kamili ya mijengo iliyoathirika | | | Kshs 350,948,460.00 |
| **D** | **Miti na mazao yaliyoathirika** | | | |
| | Idadi kamili ya kaya zenye miti zilizoathirika | | | 967 |
| | Miti ya bidhaa za mbao (Mkangazi, Mkaratusi, Mpaina, | | | 44,431 |

| No | Vitu | Nambari |
|---|---|---|
| | mti wa gravellia, Mvinje, Ober', 'Ciala, n.k) na miti ya matunda (Maembe Parachichi, mapera, Paipai nk') | |
| | Idadi kamili ya kaya zenye miti zilizoathirika | 71 |
| | Idadi kamili ya miti iliyoathirika | mazao mbali mbali |
| | Thamani kamili ya miti iliyoathirika | Kshs 71,209,016.00 |
| | Thamani kamili ya mazao yaliyoathirika | Kshs 793,700.00 |
| **E** | **Biashara zilizoathirika** | |
| | Idadi kamili ya kaya zenye biashara zilizoathirika | 49 |
| | Idadi kamili ya biashara zilizoathirika | 56 |
| | Thamani kamili ya biashara zilizoathirika | Kshs 7,489,000.00 |
| **F** | **Makaburi** | |
| | Idadi kamili ya kaya zenye makaburi yaliyoathirika | 181 |
| | Idadi kamili ya makaburi | 546 |
| | Thamani kamili ya makaburi yaliyoathirika | Kshs 81,900,000.00 |
| **G** | **Jumla ya gharama za mradi wa MMU III pamoja na asilimia kumi na tano (15%) utekelezaji na asilimia kumi (10%) gharama** | **Kshs. 948,241,218.00** |

## 1.23 Utafiti wa thamani

Ufuatiliaji utafanywa kila wakati na wakala wa utekelezaji ambaye atakusanya na kurekodi habari ya shughuli za MUU na kuwasilisha ripoti za ufuatiliaji, kwa wakati unaofaa kwa kitengo cha Usimamizi wa mradi. Mfumo wa jumla wa ufuatiliaji wa ndani utajumuisha mtiririko wa habari uanoendelea kutoka ngazi ya kaunti ndogo kupitia Kuratibu kamati za kata za uhamishaji na fidia, Kaunti za uhamishaji na Fidia za kaunti za kaunti ndogo hadi kwa bodi ya kitaifa ya umwagiliaji / unyunyizaji / mradi wa umwagiliaji wa Lower Nzoia/ kitengo cha kusimamia mradi na kufuatana na usimamizi wa mara kwa mara na uhakiki kutoka kitengo cha kusimamia mradi. Mchakato wa ufuatiliaji utahusisha ufuatiliaji wa ndani na nje.